


UKURASA 7

**SHERIA UCHAGUZI** Wadau waibua hoja elimu ya mpigakura na waangalizi

UKURASA 3

**TIC** yasajili miradi dola bilioni 560

UKURASA 4



**KESI** mauaji ya kimbari Ukanda wa Gaza yaanza kusikilizwa rasmi

UKURASA 5

Nipashe
Ijumaa Januari 12, 2024 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
MWANGA WA JAMII
ISSN 0856 • Na. 0581553
www.ippmedia.com
LIKE & FOLLOW US
www.twitter.com/nipashetz
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper

# Mzozo askari misitu, raia wajeruhi wawili

UKURASA 2



Mabaki ya damu nje ya bucha anayofanya kazi kijana Samson Lugendo (picha ndogo) anayedaiwa kujeruhiwa kwa risasi na askari wa wakala wa misitu, katika eneo la Machinjioni Tegeta, kata ya Wazo, Dar es Salaam jana . Picha ndogo: Maganda ya risasi zinazodaiwa kutumika.
**PICHA: TUNTULE SWEBE**

# Mwinyi ajivunia ongezeko ukusanyaji mapato Z' bar

UKURASA 3

Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi akimtunuku Nishani ya Mapinduzi kwa Viongozi wenye sifa za kipekee, Rais Dk. Samia Suluhu Hassan wakati wa shamrashamra za maadhimisho ya miaka 60 ya Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar katika viwanja vya Ikulu, jijini Zanzibar jana.
**PICHA: IKULU**



UKURASA WA 11

## MAENDELEO MAKUBWA ELIMU MIAKA 60 YA MAPINDUZI Z'BAR

ELIMU ni msingi mkuu wa maendeleo ya kijamii na kiuchumi. Kwa kutambua hilo, mara baada ya Mapinduzi...

## Mtoto wa mchungaji adaiwa kujinyonga kwa ugomvi wa pipi

UKURASA 2

**MICHEZO** RAIS SAMIA ACHANGIA SHILINGI MILIONI 500 KWA TIMU ZA TAIFA UK. 24

**KATUNI** UK. 6



Waziri Mkuu Kassim Majaliwa akipata maelezo kutoka kwa Mhudumu kwenye Hospitali ya Wilaya ya Kaskazini "B"-Pangatupu, Zuhura Juma Makame kuhusu mashine ya kusaidia watu wenye matatizo ya moyo, baada ya kuizindua hospitali hiyo jana, ikiwa ni sehemu ya shamrashamra za maadhimisho ya miaka 60 ya Mapinduzi ya Zanzibar. **PICHA: OWM**

# Mzozo askari misitu, raia wajeruhi wawili

**Tuntule Swebe na Beatrice Shayo**

MVUTANO kati ya vijana wanne na askari sita wa Uhifadhi wa Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS), uliobuka jana asubuhi katika eneo la Tegeta Machinjioni, mkoani Dar es Salaam, umesababisha watu wawili kujeruhiwa kwa panga na risasi.

Ushuhuda na ufuatiliaji wa Nipashe, ulibaini walikuwa wakifukuzana kutoka barabara ya Bagamoyo, ndipo askari wakahisi watuhumiwa hao waliko, wakavamia eneo hilo na katika nyendo za msako wao pasipo kuuliza na kuangukia kwenye mapambano.

Ilielezwa kuwa baada ya askari hao kuwahisi vijana wanaodaiwa si wahusika bali ni wauza mkaa, msuguano ulitokea na ghafla wakaonekana vijana wengine wakikimbia wananyoshewa kidole kwamba ndio wahusika.

Katika harakati za askari hao kubadili mwelekeo wa kuwafuatilia wahusika, askari mmoja mwenye silaha alidondoka na mtuhumiwa mmoja kabla ya kutoweka hapo, alimkata na panga mgongoni. Hilo lilitokea, huku wanaodaiwa kuwa wahusika wakitoweka eneo hilo kwa kukimbia.

Baada ya tukio hilo la kujeruhiwa askari, askari mwingine mwenye bunduki, baada ya kuona hali hiyo, 'akajibu mapigo' kwa kufyatua risasi ambayo ilikwenda moja kwa moja kwa kijana mwingine muuza nyama (buchani) na kumjeruhi kichwani.

Ghafla askari waliobaki wa TFS walitoweka, huku raia wema waliokuwapo wakiwapeleka majeruhi hospitali kwa matibabu.

Nipashe ikadokezwa kwamba kijana huyo yuko Hospitali ya Kitengule huku askari akipelekwa Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH) kutokana na hali yake.

Pia msuguano huo ulifanyika katika eneo jirani na mahali pa kuuzia mkaa ambako Nipashe ilipohoji wahusika walikataa kuhusika kwa namna yoyote na tukio hilo lililotokea saa 2:30 asubuhi, kwa kuwa walikuwa hawajafungua shughuli zao.

Mjumbe wa Mtaa wa Machinjioni, Salum Mketo, aliyekiri kuwa shuhuda wa sakata hilo, alisema wakati gari la TFS linafika katika eneo hilo, askari wake walienda palipo na kibanda cha mkaa na kutawanyika.

"Kuna wengine walienda kibanda cha mkaa na kutawanyika na walipofika kwenye bucha ya nyama kukawa na mzozo. Mimi nilikuwa pembeni ninatizama tangu gari lilipofika na wanavyofanya askari wa maliasili wakapiga risasi na kumjeruhi kijana huyo," alisema.

Mjumbe huyo alieleza kushangazwa kwake na staili iliyotumiwa na askari hao ambao hawakufuata taratibu huku wakitumia nguvu kubwa wakijipa uenyeji wa eneo bila kuwashirikisha wajumbe.

"Hawakutaka msaada kwa Mjumbe wala serikali ya mtaa na kujitambulisha. Wanachokitaka ni kipi? Ni kawaida yao na ni mara ya nne wanakuja nawatazama tu," alisema Mketo.

Mwenyekiti wa Serikali ya Mtaa wa Wazo, Medard Mashauri, alipozungumza na Nipashe kwa njia ya simu, alikiri kupokea simu ya raia mwema aliyemjulisha taharuki iliyojitokeza eneo lake la Machinjioni.

Alisema watu wa hifadhi wa misitu walikuwa wanawafuatilia wafanyabiashara wa mkaa ambao ni watu wanne.

"Hao wafanyabiashara walinukuliwa na wananchi wakisema 'tumewachoka usiku kucha tulikuwa nao huko porini mnatufuata mpaka huku. Tumechoka, bora tufe sasa tuuane' hayo ndio maneno waliyosema hao wafanyabiashara, mimi sikuwapo nimeambiwa na wananchi wangu.

"Basi wale wafanyabiashara wakachomoa mapanga, wale huwa wanatembea na mapanga (anataja kabila lao) na katika gari kulikuwa na askari sita. Kati yao, watatu walikuwa na bunduki, mmoja alikuwa na panga na mwingine alikuwa na fimbo.

"Na ndani ya gari alibaki askari mmoja. Wale wafanyabiashara wakaanza kurusha mawe, ikabidi yule askari akaliwasha gari na kulitoa katika lile eneo," alisimulia Mwenyekiti huyo.

Alisema baada ya gari hilo kuondoka, askari waliobaki chini wafanyabiashara waliwafuata na wao wakaanza kurudi nyuma, ndipo askari mmoja alianguka na bunduki yake na kushambuliwa kwa panga.

"Wafanyabiashara wakaanza kumshambulia. Nimeambiwa huyo askari kaumia na amepelekwa Muhimbili na mwananchi wangu amejeruhiwa kwa kupigwa risasi kichwani akiwa buchani kwake na kwa sasa anapatiwa matibabu Hospitali ya Kitengule," alisema.

Nipashe ilipozungumza na mtu aliyejitambulisha kuwa 'ndugu wa majeruhi buchani' aliyekuwa akikusanya maganda ya risasi kwa ajili ya kupeleka polisi, alimtambulisha majeruhi kuwa ni Samson Lugendo (26).

Mmoja wa mashuhuda wa tukio hilo, Thomas Jeremiah, alisimulia kuwa aliona askari wamevamia stoo za mkaa wakaanza kukagua kwa madai wanatafuta wasafirishaji mkaa waliokuwa na bodaboda.

"Ndipo walipoanza kukimbizana, ghafla na askari wakarusha risasi na kwenda kumpata Lugendo (muuza nyama) akiwa katika biashara zake," alisema Jeremiah.

Kalisto Raphael, anayeuza mkaa mahali hapo, alisema waliokuwa wakitafutwa, hawakushusha mkaa katika eneo hilo, bali walikimbilia hapo. "Wale askari walikuwa wanawakimbiza wanaosafirisha mkaa, walivyofika hapa hawakuwaona na kuanza kufanya msako.

"Ghafla ikatokea taharuki, ndipo askari wa Maliasili aliposhambuliwa na askari wa Maliasili (mwingine) kurusha risasi, ikampata mtu ambaye hahusiki na masuala ya mkaa," alisema Raphael.

Mkuu wa Wilaya ya Kinondoni, Saad Mtambule, aliyekuwapo hospitalini Kitengule, alimwambia mwandishi wa Nipashe aliyekuwa akifuatilia hatua zote za tukio hilo, alipotakiwa kufafanua, akajibu kwa kifupi, "majeruhi hao wapo hospitali wanaendelea na matibabu".

Nipashe ilipomtafuta Mtendaji Mkuu wa TFS, Profesa Dos Santos Silayo, jana jioni alikiri askari wake kujeruhiwa kwa mapanga na yupo katika hali mbaya.

"Kama kuna mtu mwingine amejeruhiwa kwa risasi ni mambo yanayotengenezwa, ila sijui kama kuna ukweli tunaendelea kufuatilia.

"Maana hakuna kilichoonekana tangu asubuhi mpaka muda huu ndio nasikia kuna malalamiko ya mtu kupigwa risasi au kuumia katika vurugu hizo. Kujeruhiwa mtu ambaye yupo mbali na tukio bado sijaelewa limekuwaje, hilo tunaendelea kufuatilia," alisema Silayo.

Alilalamika kuwapo njama za stoo za kuhifadhi mikaa haramu zinazozuia mazingira ya utendaji wao kudhibiti usafirishaji haramu wa mkaa, ila kwa mkasa wa jana aliahidi kufuatilia kwa ushirikiano na polisi.

## Mtoto wa mchungaji adaiwa kujinyonga kisa pipi

**Na Jaliwason Jasson,** MANYARA

MTOTO wa Mchungaji wa Kanisa la Mungu Tanzania, Tawi la Mtaa wa Bagara Ziwani, Babati mkoani Manyara, Bright Laizer, amedaiwa kujinyonga kwa kutumia kamba ya kufungia mbuzi na fulana yake huku akiacha ujumbe wa maandishi ya wino mwekundu kumwomba msamaha mama yake.

Akizungumzia tukio hilo, Mwenyekiti wa Mtaa wa Bagara Ziwani, John Konki, alisema tukio la mtoto huyo mwenye umri wa miaka tisa, lilitokea majira ya saa 7:45 mchana nyumbani kwao.

Wakati tukio hilo likiwa limetokea, Kamanda wa Polisi Mkoa wa Manyara, Kamishna Msaidizi (ACP) George Katabazi, amesema hajapata taarifa za tukio hilo.

Konki alisema tukio hilo ni la kusikitisha mtoto wa miaka tisa kujitoa uhai wake katika mazingira ya namna hiyo.

Alisema alipopata taarifa za mtoto huyo kujinyonga, alifika nyumbani kwao na alipoingia ndani alimkuta baba yake amemtoa kwenye kamba akiendelea kumpa huduma ya kwanza.

Alisema walikuta mtoto ameandika ujumbe kwenye karatasi ukisema: "Mama naomba unisamehe nimeamua kujiua kwa sababu dada ndio amesababisha."

Konki alisema baada ya kumkuta baba yake akimpa huduma ya kwanza bila mafanikio, aliwapigia polisi kuwapa taarifa na walipofika wakambeba kwa gari lao na kumpeleka Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Manyara ili kuona namna ya kumnusuru kwa sababu waliona bado yuko hapo.

Kuhusu baba yake, alisema Mchungaji Ezekiel Laizer ameishi naye miaka mitatu ila ni mtu mwema, anapenda watu na hajawahi kuona anampiga mtoto maana anapenda sana watoto.

Dada wa marehemu huyo, Beatrice Laizer (15), akisimulia kisa hicho, alisema mdogo wake alichukua kitu chake, alipomhoji alimjibu kuwa hajakichukua.

NIPASHE ilipomhoji ni kitu gani alidai ni pipi maarufu kama Kaksi ambayo baada ya Bright kukana kuchukua, wakawa na majibizano makali na alipoingia chumbani kwake aliaga anaenda kujisomea.

Alisema ghafla baba yao alirudi nyumbani na kuuliza aliko Bright, alipoelekezwa kuwa yuko chumbani anajisomea. Baba huyo aliingia na kukuta amejinyonga kwa kamba ya mbuzi na fulana yake huku mwili wake ukining'inia.

Dada mwingine anayeishi nyumbani hapo, Rahel Laizer, alisema alipomaliza kula chakula alikwenda kulala na kumwacha Beatrice akimwuliza Bright kwa kuchukua pipi baada ya kukataa ghafla kimya kilitanda.

Mmoja wa majirani, Veronica Sulle, alisema taarifa za mtoto huyo kujinyonga alipewa na mfanyakazi wake baada ya kusikia kelele za watoto wakilia.

Alisema mtoto huyo alikuwa mcheshi, mpole sana ambaye alikuwa anacheza na mjukuu wake.

## HABARI KITAIFA

# Mwinyi ajivunia ongezeko ukusanyaji mapato

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, amesema makusanyo ya mapato visiwani humo yameongezeka hadi kufikia Sh. trilioni 1.4 mwaka 2022/23 kutoka Sh. bilioni 790.48 mwaka 2020/21, sawa na ongezeko la asimilia 56.4.

Katika hotuba yake jana ya maadhimisho ya miaka 60 ya Mapinduzi Zanzibar, Dk. Mwinyi alisema kasi ya ukuaji wa uchumi mwaka 2022 imefikia wastani wa asilimi 6.8 ikilinganishwa na asilimia 1.3 ya mwaka 2020.

"Kiwango cha ukuaji wa uchumi wetu ni kikubwa ikilinganishwa na nchi nyingi zinazoendelea," alisema.

Alisema thamani ya Pato Halisi la Taifa (GDP) imeongezeka kutoka Sh. trilioni 3.116 kwa mwaka 2020 na kufikia thamani ya Sh. trilioni 3.499 mwaka 2022.

"Kukua kwa uchumi wetu kumetokana na kuongezeka kwa uwekezaji kwa kutekelezwa miradi ya maendeleo ya kipaumbele ikiwamo miundombinu ya barabara, bandari, viwanja vya ndege, huduma za maji safi na salama, uimarishaji wa huduma za nishati ya umeme, masoko na kuimarika kwa sekta ya huduma kwa kuongezeka kwa idadi ya watalii," alisema.

Rais Mwinyi alisema pato la mtu binafsi nalo limeongezeka kutoka Dola za Marekani 1,099 sawa na milioni 2.5 mwaka 2020 na kufikia Dola 1,230 sawa na milioni 2.8 mwaka 2022.

"Jitihada zilizochukuliwa na serikali zimeweza kudhibiti kasi ya mfumuko wa bei na kuendelea kuwa katika tarakimu moja. Kwa mwaka 2023 mfumko wa bei ulikuwa wastani wa asilimia 6.8 hali inayomhakikishia mwananchi kupata mahitaji ya lazima," alisema.

Rais Mwinyi alisema serikali za awamu zote zilizopita baada ya Mapinduzi, zilichukua juhudi za uwekezaji kwa ujenzi wa miundombinu, majengo ya ofisi, huduma na makazi, viwanda na kuwakaribisha wawekezaji kuzitumia fursa na rasilimali zilizoko nchini katika kuchangia ukuaji wa uchumi.

"Tunapoadhimisha miaka 60 ya Mapinduzi na miaka mitatu ya Serikali ya Awamu ya Nane, tumeshuhudia mafanikio makubwa katika jitihada zetu za kuvutia wawekezaji," alisema.

Kasi ya uwekezaji nchini, alisema imeongezeka ambapo jumla ya miradi 296 yenye thamani ya Dola bilioni 4.5 imeidhinishwa.

Alisema miradi hiyo inakadiriwa kutoa ajira zipatazo 17,479, ikihusisha uwekezaji katika visiwa vidogo 16 wenye thamani ya Dola milioni 377.5, ujenzi wa hoteli za kitalii 112, viwanda 36, biashara ya majengo 56 na miradi mingine ya kiuchumi.

Alisema mafanikio haya yametokana na mageuzi makubwa yaliyofanywa na serikali ikiwamo uimarishaji wa huduma zinazotolewa na Mamlaka ya Kukuza Uwekezaji Zanzibar (ZIPA) na sasa wawekezaji wanaweza kupata huduma zote za uwekezaji katika kituo kimoja (One Stop Center) ndani ya masaa 24.

Rais Mwinyi alisema serikali inaendelea kuchukua hatua za kuvutia wawekezaji ikiwa ni pamoja na kutangaza fursa zilizopo katika maeneo ya bandari jumuishi ya Mangapwani na ujenzi wa miundombinu ikiwamo barabara, maji na umeme katika maeneo ya uwekezaji.

"Kwa kuzingatia umuhimu wa biashara kwa Zanzibar, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imechukua hatua mbalimbali kuimarisha mazingira ya ufanyaji wa biashara. "Tunapoadhimisha miaka 60 ya Mapinduzi na mitatu ya Serikali ya Awamu ya Nane, sekta ya biashara ya usafirishaji na uingizaji bidhaa kwa ujumla inaendelea kuimarika ambapo kwa mwaka 2022, Zanzibar imefanya biashara yenye thamani ya trilioni 1.4 ukilinganisha na trilioni 913.1 kwa mwaka 2020, sawa na ongezeko la asilimia 57.6," alibainisha.

Rais Mwinyi alisema Zanzibar imesafirisha nje bidhaa zenye thamani ya Sh. bilioni 180.4 kwa mwaka 2022, sawa na ongezeko la asilimia 174.7, ikilinganishwa na usafirishaji wa bidhaa zenye thamani ya Sh. bilioni 65.7 kwa mwaka 2020.

"Kwa mwaka 2022, Zanzibar imesafirisha tani 6,452.8 za karafuu yenye thamani ya Sh. bilioni 118.3, ikilinganishwa na tani 3,506.8 zilizosafirishwa mwaka 2020, zenye thamani ya Sh. bilioni 38.37, sawa na ongezeka la fedha la asilimia 208.1.

"Kwa upande wa seaweed, Zanzibar imesafirisha tani 13,972.5 zenye thamani ya Sh. bilioni 16.0 kwa mwaka 2022, ukilinganisha na tani 11,382.6 wenye thamani ya Sh. bilioni 11.7 kwa mwaka 2020, sawa na ongezeko la asilimia 36.8," alisisitia.

Kuhusu biashara baina ya Zanzibar na Tanzania Bara, mwaka 2022, Zanzibar imesafirisha bidhaa zenye thamani ya Sh. bilioni 37.64, ikilinganishwa na bidhaa zenye thamani ya Sh. bilioni 15.03, zilizosafirishwa mwaka 2020.

Kuhusu uagizaji bidhaa katika kipindi cha mwaka 2022, alisema Zanzibar imeagizia bidhaa zenye thamani ya Sh. bilioni 375.80 kutoka Tanzania Bara ikilinganishwa na uagiziaji wa bidhaa zenye thamani ya Sh. bilioni 243.81 kwa mwaka 2020.

Alisema kwa madhumuni ya kuleta mapinduzi ya kiuchumi, serikali imechukua hatua za kuimarisha uwezeshaji wa wananchi kiuchumi na kupambana na umaskini.

"Serikali imepata mafanikio katika uimarishaji wa vikundi vya ushirika ambapo jumla ya vikundi 1,546 vya ushirika vimesajiliwa. Idadi hiyo imewezesha kufikia vikundi 3,662 vya ushirika vilivyosajiliwa nchini.

# Wadau waibua hoja kuhusu elimu mpigakura, watazamaji uchaguzi

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

MASHIRIKA 27 yanayofahamika kwa umoja wao kama Ushiriki Tanzania, yamependekeza uwapo wa sura mpya ya elimu kwa mpigakura na watazamaji wa uchaguzi kwenye sheria ya uchaguzi.

Mwenyekiti wa umoja huo, Israel Ilunde, alisema hayo jana jijini hapa wakati akiwasilisha mapendekezo hayo mbele ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria kuhusu miswada minne ya sheria za uchaguzi ya Tume ya Taifa ya Uchaguzi.

"Muswada wa Sheria ya uchaguzi kwa urais, wabunge na madiwani umekosa sura yenye vifungu maalum vinavyoonyesha mambo yanayohusiana na elimu ya mpiga kura.

"Tumependekeza kifungu kipya kisomeke Tume ya Taifa ya Uchaguzi katika kutekeleza majukumu yake kwa mujibu wa sheria, hii itaweka utaratibu wa elimu endelevu ya mpiga kura na kuandaa mtaala wa elimu ya mpiga kura kwa kushirikiana na taasisi asasi na makundi mengine ya kiraia," alisema.

Alisema kifungu kingine walichopendekeza ni mtaala wa elimu ya mpigakura utakaoandaliwa utashirikisha taasisi, asasi na makundi mengine ya kiraia katika kutoa elimu ya mpiga kura.

"Kifungu kidogo ya tatu madhumuni ya kifungu hiki Tume itazingatia sifa zifuatazo katika kualika na kusajili taasisi, asasi na makundi mengine ya kiraia kwa ajili ya kutoa elimu ya mpiga kura taasisi au asasi inapaswa kuwa imesajiliwa na kufanya kazi kwa mujibu wa sheria, uwezo wa kuwafikia wapiga kura ikiwamo makundi maalum kama watu wenye ulemavu wanawake na vijana,"alisema.

Aidha, alisema maombi ya utoaji wa elimu ya mpiga kura yatawasilishwa kwa njia ya maandishi ya nakala ngumu na nakala tepe ndani ya siku 21 tangu kutolewa tangazo la mwaliko wa kutoa elimu ya mpigakura.

Alisema kifungu kingine kinasema ndani ya siku 30 baada ya muda wa maombi uliopangwa kuisha, Tume itatangaza orodha ya watakaoshiriki kutoa elimu ya mpigakura.

"Taasisi ambayo maombi haijaridhiwa na maombi, kukata rufaa katika mahakama ya wilaya au mahakama ya rufani ndani ya siku 14 baada ya Tume kutangaza orodha ya watakaoshiriki kutoa elimu ya mpiga kura,"alisema.

Ilunde alisema sehemu ya pili ya pendekezo hilo ni watazamaji wa uchaguzi na wamependekeza Tume katika kutekeleza majukumu yake kwa mujibu wa sheria hiyo, itaweka utaratibu wa kualika na kusajili watazamaji wa uchaguzi na itashirikiana na taasisi,asasi na makundi mengine ya kiraia kuandaa mwongozo wa kusimamia watazamaji wa uchaguzi.

Alisema utaratibu utakaoandaliwa utafanyika kwa kushirikisha taasisi, asasi na makundi mengine ya kiraia.

"Kwa madhumini ya kifungu hiki, tume itasimamia sifa zifuatazo kwa ajili ya kusajili watazamaji wa uchaguzi taasisi ama asasi lazima iwe imesajili na inafanya kazi kwa mujibu wa sheria.

"Iwe na uwezo wa kufuatilia mchakato wa uchaguzi na kuyafikia maeneo ya kijiografia bila kuathiri masharti yaliyopo kwenye kifungu hicho, maombi ya kuomba kuangalia uchaguzi yatawasilishwa kwa njia ya maandishi ya nakala ngumu na nakala tepe ndani ya siku 21 tangu kutolewa kwa tangazo," alisema.

Dk. Mzuri Issa kutoka Chama Waandishi wa Habari Wanawake Tanzania (TAMWA) Zanzibar, alisema wamependekeza kifungu kipya kinachozungumzia masuala ya usalama na ulinzi wakati wa uchaguzi.

Alisema kifungu hicho kinatokana na sababu kuwa wanawake wengi pamoja na watu walipo kwenye makundi maalum wana wasisi na vurugu za uchaguzi.

"Tunaomba sana hichi kifungu mheshimiwa mwenyekiti kiwapo pia, tumesema kwa mujibu wa kifungu hichi kutakuwa na polisi maalum wa uchaguzi na jeshi la polisi tu ndilo likalohusika na usalama wakati wa uchaguzi na tume ndiyo itateuwa kikosi hicho maalum na kwa kushirikiana na Jeshi la Polisi.

"Hii ni kwa sababu wakati mwingine zinatokea vurugu hajulikani nani ambaye aliyefanya zile vurugu, hata mazungumzo yetu sisi na polisi wanasema sisi siyo tuliyofanya zile vurugu kwa hiyo, kuna kuwa hakuna mtu anayebea hilo jukumu," alisema.

Pia alisema kifungu cha nne kinasema kwa ajili ya kulinda makundi maalum Jeshi la Polisi itakuwa linasajili matokeo ya matukio yote ya ukatili na uzalilishaji dhidi ya makundi haya na Tume itachua hatua kwa kila kosa ikiwamo kufanya uchunguzi.

Hata hivyo, alisema hali hiyo itasaidia kuondoa hofu ambazo zimekuwa zikitokea kwa watu wenye mahitaji maalum, wanawake pamoja na vijana kuhusu vurugu kwenye uchaguzi.

Victoria FINANCE

Victoria Finance Plc
5th Floor, Mwanga Tower Building-Kijitonyama
New Bagamoyo Road
P.O.Box 12102, Dar es Salaam - Tanzania
Telephone +255 22 277 4577
Fax: +255 22 277 4559
Email: info@victoriafinance.co.tz
Website: www.victoriafinance.co.tz

**TANGAZO LA MINADA YA HADHARA**

VICTORIA FINANCE PLC INAPENDA KUUTANGAZIA UMMA YA KWAMBA KWA IDHINI ITAKAYOTOA KWA KAMPUNI TOFAUTI ZA UDALALI INATARAJIA KUUZA KWA MNADA WA HADHARA DHAMANA ZA WADAIWA SUGU KAMA IFUATAVYO;

| NA. | JINA LA MDAIWA | DHAMANA | NYARAKA YA UMILIKI NA SEHEMU | DALALI | TAREHE |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | KHALFAN NASSORO ABEID | NYUMBA | LESENI YA MAKAZI – MANZESE B, KILOSA | J&J RECOVERIES | 24/01/2024 |
| 2 | RASHID ATHUMAN MGAYA | NYUMBA | LESENI YA MAKAZI- DAKAWA, MVOMERO | J&J RECOVERIES | 24/01/2024 |
| 3 | MOSES ANDREW ODUNGA AKIWA MSIMAMIZI WA MIRATHI YA MAREHEMU ANDREW JUMA ODUNGA | NYUMBA | HATI MILIKI- NJIRO, ARUSHA JIJI | J&J RECOVERIES | 17/01/2024 |

Minada yote itafanyika mahali husika katika muda na siku ambayo itatangazwa kupitia katika vipeperushi na magari ya matangazo kutokana na idhini itayotoka kutoka katika vyombo husika vya Serikali.

**MASHARTI YA MNADA;**

- Asilimia 25% ya bei iliyofikia italipwa papo hapo na asilimia 75% iliyosalia ilipwe ndani ya siku kumi na nne. (14). Kwa kushindwa kufanya hivyo itapelekea mnada kurudiwa tena na pesa zilizolipwa kutokurudishwa.
- Gharama za kumuhamisha mmiliki na kubadili umiliki ni juu ya mnunuzi.
- Dhamana itauzwa Kama ilivyo.

# TIC yasajili miradi ya dola bilioni 560/-

**Na Joseph Mwendapole**

KITUO cha Uwekezaji Tanzania (TIC) kimesajili miradi 504 kwa mwaka 2023 yenye thamani ya Dola za Marekani bilioni 560 ambayo kukamilika kwake kutasaidia kuzalisha ajira 230,000.

Aidha, serikali imekipa kituo hicho lengo la kusajili miradi yenye thamani ya Dola za Marekani bilioni 15 ambazo ni sawa na Sh. trilioni 35 ifikapo mwaka 2025.

Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais (Mipango na Uwekezaji), Prof. Kitila Mkumbo, alisema hayo jana Dar es Salaam wakati akizungumza na waandishi wa habari katika ofisi za TIC.

Prof. Mkumbo alikuwa akizungumza kuhusu kampeni ya kitaifa ya kuhamasisha uwekezaji wa ndani ambayo imeanza Januri na inatarajiwa kihitimishwa mwezi Septemba mwaka huu.

Mkumbo alisema kupitia utekelezaji wa Sera na Sheria, serikali imeendelea kupata mafanikio mbalimbali katika kuhamasisha, kuvutia na kuwezesha uwekezaji nchini.

Pia alisema hivi karibuni Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, alizindua rasmi kampeni ya kitaifa ya kuhamasisha uwekezaji kwa lengo la kutoa msukumo maalum kwa watanzania kuchangamkia fursa za uwekezaji zilizoko nchini.

Alisema kama sehemu ya utekelezaji wa kampeni hiyo, Ofisi ya Rais Mipango na Uwekezaji imeamua kuufanya mwaka 2024 kuwa mwaka wa kitaifa wa kuhamasisha uwekezaji nchini hasa kwa watanzania.

Katika kutekeleza mpango huo, alisema kuanzia Januari hadi Februari, mwaka huu, ofisi yake kwa kushirikiana na TIC wataendesha kampeni maalum nchi nzima kupitia vyombombalimbali vya habari.

Alisema baada ya kukamilika kwa kampeni ya vyombo vya habari, kampeni hiyo itaendelea kwa mwaka mzima kupitia semina na makongamano katika mikoa na wilaya zote nchini na kwamba itahitimishwa na kongamano la kitaifa la uwekezaji.

Kwa mujibu wa Waziri, kampeni hiyo ina malengo saba mahususi ya kutoa elimu ya uwekezaji kwa watanzania ikiwemo kuondoa dhana kwamba uwekezaji ni kwaaajili ya wageni na kwamba ili uwekeze lazima uwe tajiri.

Kampeni hiyo, alisema itasaidia kuwaelimisha wananchi kuhusu taratibu za kusajili miradi ya uwekezaji kupitia TIC na kuwaeleza kuhusu vivutio mbalimbali vya kikodi na visivyo vya kikodi.

Alisema vivutio hivyo vinatolewa kwa wawekezaji wa ndani na nje wanaposajili miradi kupitia TIC lakini uzoefu umoenyesha kwamba watanzania wengi hawavijui.

Pia alisema kwenye kampeni hiyo pia wataonyesha mafanikio ambayo watanzania wameyapata na kuonyesha fursa zilizopo pamoja na kupokea changamoto zinazowakabili watanzania kwenye uwekezaji na kuzitatua.

Prof. Mkumbo alisema kampeni hiyo itatumika kukuza ushirikiano na wakuu wa mikoa, wakuu wa wilaya, wakurugenzi wa mamlaka za serikali za mitaa na viongozi wa sekta binafsi ili watumie fursa za uwekezaji kwenye maeneo yao.

Mkumbo alisema malengo mahsusi ya serikali katika kuhamasisha, kuvutia na kuwezesha uwekezaji ni kuvutia mitaji na teknolojia mpya nchini kutoka mataifa mengine yaliyopiga hatua kiteknolojia.

"Matokeo ya uwekezaji katika nchi hujitokeza katika kuongeza ajira, kuongeza mapato ya kodi, kupunguza uagizaji wa bidhaa kutoka nje na kuongeza mauzo ya bidhaa zilizoongezwa thamani nje ya nchi kwa ujumla uwekezaji ni nyenzo muhimu katika kukuza uchumi na kuleta maendeleo," alisema.



Makamu wa Kwanza wa Rais Zanzibar, Othman Masoud Othman (wa nne kulia) akizindua mradi wa ujenzi wa nyumba za makazi 240 wa The Soul, unaosimamiwa na kampuni ya CPS Afrika, eneo la Paje, Mkoa wa Kusini Unguja jana, uwekezaji unaotengeneza fursa za kuendeleza utalii na kukuza uchumi nchini. Wa (nne kushoto) ni Ofisa Mkuu wa Biashara wa CPS Afrika, Tobias Dietzold. **PICHA: MPIGAPICHA WETU.**

# Wateule wa Rais wapewa mbinu kutotenguliwa

**Na Jenifer Gilla**

UTEUZI na kutenguliwa baadhi ya wakuu wa taasisi, viongozi wa serikali na bodi mbalimbali unaofanywa kila mara na Rais Samia Suluhu Hassan, umewaibua wadau na kuwashauri wanaoteuliwa kufanyia kazi kasoro za wenzao wanaoondolewa ili kudumu katika nafasi hizo.

Wadau hao wamesema kutokana na ushauri huo, itampunguzia mzigo Rais wa kuteua na kutengua viongozi.

Wakati ushauri huo ukitolewa, juzi Rais Samia alitengua uteuzi wa Mtendaji Mkuu wa Wakala wa Mabasi Yaendayo Haraka (DART), Dk. Edwin Mhede, na nafasi yake kuchukuliwa na Dk. Athuman Kihamia.

Utenguzi huo umekuja wakati kukiwa na malalamiko ya wananchi kuhusu huduma mbovu ya usafiri wa mwendokasi ikiwamo abiria kukaa vituoni muda mrefu.

Mwezi uliopita Rais Samia pia, alivunja Bodi ya Wakurugenzi ya Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) na kumteua Dk. Rhimo Simeon kuwa Mwenyekiti wa Bodi hiyo akichukua nafasi ya Meja Jenerali Paul Kisesa, aliyeteuliwa kuwa Balozi wa Tanzania nchini Uganda.

Mabadiliko hayo yalifanyika ikiwa ni miezi mitatu tangu alipobadilisha nafasi ya mkurugenzi mtendaji katika taasisi hiyo na kumteua Mhandisi Gissima Nyamo - Hanga, akichukua nafasi ya Maharage Chande aliyemteua kuwa Postamasta Mkuu wa Shirika la Posta Tanzania (TPC).

Katika maoni ya wadau hao waliyoyatoa jana, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) mstaafu, Ludovick Utouh, alisema mabadiliko katika taasisi hizo ni suala lisilokwepeka, ikiwa aliyeteuliwa ataonyesha udhaifu katika utendaji kazi wake.

Alisema Rais anateua kiongozi akiamini kuwa ana uwezo wa kutekeleza majukumu atakayowapangia, hivyo inapotokea mtu huyo kushindwa kuleta matokeo tarajiwa katika taasisi husika, ana wajibu wa kumtengua na kuteua mwingine ambaye anaamini atafanya kazi nzuri.

"Mabadiliko wakati mwingine hayakwepeki kwa sababu mfumo ndio unamteua mtu kwa kuamini kwamba atatekeleza majukumu yake kama inavyotarajiwa. Akienda pale akapwaya maana yake, hujaweza kutimiza matarajio ya Watanzania," alisema.

Utouh ambaye ni Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi ya WAJIBU alisema ili kuzuia mambo haya kutokea mara kwa mara, wanaoteuliwa kushika nafasi hizo wanapaswa kuangalia kilichosababisha wenzao watolewe na kukifanyia kazi.

Mwanadiplomasia, Hamduni Maliseli, alishauri timu inayompelekea Rais majina ya viongozi wa kuwateua katika taasisi zifanye uchunguzi wa kina kwa watu hao ili kuepuka kuweka watu katika taasisi ambazo hawana elimu na weledi wa kutosha kuzisimamia.

"Hizi kamati za Waziri Mkuu (Kassim Majaliwa) na nyingine zinazompelekea Rais majina ya wateule zinapaswa kuwajadili hawa watu kwa kina na kujiridhisha kuwa, wana uwezo wa kutekeleza majukumu na kutoa matokeo tarajiwa katika nafasi hizo," alisema.

Alisema tatizo kubwa ni kwamba wanaoteuliwa kushika nafasi hizo, wanakosa uvumbuzi na ubunifu wa kutosha kukabiliana na changamoto wanazokutana nazo katika taasisi hizo.

"Rais ana wajibu wa kumtengua kiongozi aliyemteua pale anapoona ameshindwa kusimamia sera na utendaji katika eneo alilokutuma ili kuboresha huduma za kijamii na kuondoa kero zilizopo," alisema.

# Zimamoto yazidi kusaka mwili uliosombwa na maji

**Na Christina Haule,** MOROGORO

JESHI la Zimamoto na Uokoaji Mkoa wa Morogoro, limeendelea na harakati kwa siku ya pili kuutafuta mwili wa Mwanahamisi Issa (35), mkazi wa Bigwa, Manispaa ya Morogoro, bila mafanikio.

Mwanahamisi ni mmoja wa wanafamilia wanne waliosombwa na maji baada ya mvua kunyesha.

Tukio hilo la wanafamilia hao kusombwa na maji lilitokea juzi mkoani humo ambapo miili miwili iliopolewa, huku baba wa familia hiyo akijiokoa kwa kupanda juu ya mti.

Kamanda wa Kikosi hicho, Mrakibu Shabani Marugujo, akizungumza na Nipashe kuhusu tukio hilo, alisema juhudi za kuutafuta mwili huo zinaendelea pembezoni mwa Mto Mgolole licha ya maji kujaa yaliyotokana na mvua zilizonyesha usiku wa kuamkia jana .

Alisema tayari wameshatoa taarifa kwa wilaya na mikoa jirani unakoelekea mto huo ili watoe taarifa kama wataona kitu au mwili unaoelea kuanzia leo (jana) sababu kitaalamu mwili unaweza kuwa umeshaanza kupanda juu.

"Kama ikifika kesho (leo) na bado mwili haujaonekana basi utakuwa umefukiwa kwenye baadhi ya mashimo, michanga, miti au matope mengi yaliyokuwa yanapita katika mto huo kutokana na mvua ya usiku wa kuamkia leo (jana). Ikitokea hivyo tutaongeza jitihada za kufukua mashimo," alisema.

Akitoa taarifa za mvua za kuamkia jana, kiongozi huyo alisema wakazi wa kaya nane kwenye Mtaa wa Mafisa Mwisho katika kata ya Mafisa, mkoani humo wamepata taharuki baada ya maji kuzingira nyumba zao kuanzia saa saba usiku.

Alisema kikosi cha zimamoto na uokoaji kilifika katika eneo hilo na kuwasaidia kwa kuyatafutia njia maji hayo kwenda katika mito.

Nipashe ilishuhudia barabara ya Masika-Stendi ndogo ya daladala ya zamani kufungwa kutokana na kujaa tope na miti ambayo imesogezwa na maji mengi kutokana na mvua hiyo.

Wakazi wa Kata ya Lukobe, Manispaa ya Morogoro wameiomba serikali kuwasaidia kuboresha miundombinu ya barabara zilizopo Mtaa wa Tushikamane na Mgudeni baada ya kugeuka baada ya mvua hizo.

Mkazi wa Mtaa Tushikamane, Mwalimu Nyaonge Mkama alisema ujenzi wa mifereji katika barabara za mitaa hiyo unapaswa kuzingatiwa kwa sababu hata inaponyesha mvua kidogo barabara kujaa maji.

# Mahakama yaanza kusikiliza kesi mauaji ya kimbari Gaza

**The Hague Uholanzi**

MAHAKAMA ya Haki ya Kimataifa (ICJ), imeanza kusikiliza kesi iliyofunguliwa na Afrika Kusini dhidi ya Israel kwa madai ya kufanya mauaji ya kimbari katika Ukanda wa Gaza.

Afrika Kusini ambayo inapinga kwa kiasi kikubwa operesheni za kijeshi za Israel ndani ya Gaza, imeifungua kesi hiyo katika mahakama hiyo yenye makao yake, The Hague, Uholanzi.

Nchi hiyo inataka ICJ kuilazimisha Israel kusitisha operesheni za kijeshi Ukanda wa Gaza na kueleza inafanya mauaji ya kimbari katika eneo hilo. Pia inaitaka ICJ kuzingatia matendo ya Israel kwenye ardhi hiyo ya Wapalestina chini ya Mkataba wa Kimataifa wa Kuzuia Mauaji ya Kimbari wa mwaka 1948.

Kulingana na mkataba huo, mauaji ya kimbari ni matendo yanayosababisha vifo vya watu wengi kwa lengo la kusambaratisha kwa sehemu au kwa jumla, taifa zima, kabila au jamii ya watu wa rangi au dini moja.

Afrika Kusini na Israel zote zimetia saini mkataba huo ambao unazilazimisha kutofanya mauaji ya kimbari na pia kuyazuia na kuadhibu.

Akizungumza katika ufunguzi wa kesi hiyo, Wakili wa Mahakama Kuu ya Afrika Kusini, Adela Hassim, alisema shambulizi la Oktoba 7, mwaka jana, lililofanywa na Hamas, haliwezi kuhalalisha Israel kuvunja mkataba huo.

Rais wa Afrika Kusini, Cyril Ramaphosa, alisema hatua yao ya kupinga mauaji ya watu Ukanda wa Gaza, imewasukuma wao kama nchi kufungua kesi katika mahakama hiyo.

Hata hivyo, Israel imekanusha shutuma za kufanya mauaji ya kimbari, ikisema hazina msingi wowote na kwamba inafanya kazi kwa mujibu wa sheria za kimataifa.

Waziri Mkuu wa Israel, Benjamin Netanyahu, alisema kuwa anataka kuweka wazi kwamba Israel haina nia ya kuikalia kwa mabavu Gaza au kuwaondoa raia wake.

"Israel inapambana na magaidi wa Hamas na si idadi ya Wapalestina. Tunafanya hivyo kwa kuzingatia kikamilifu sheria ya kimataifa. Jeshi linafanya kila iwezalo kupunguza vifo vya raia, huku Hamas ikifanya kila iwezalo kuviongeza kwa kuwatumia Wapalestina kama ngao yao dhidi ya mashambulizi," alisema Netanyahu.

Mahakama hiyo imeanza kusikiliza hoja za Afrika Kusini, kabla ya kupokea majibu ya Israel leo. Uamuzi wa dharura unatarajiwa kutolewa ndani ya mwezi huu.

Hata hivyo, Mahakama hiyo haitotoa uamuzi kuhusu madai ya mauaji ya kimbari.

Wakati huo huo, operesheni za kijeshi za Israel katika Ukanda wa Gaza zimelenga mji wa kusini wa Khan Younis pamoja na kambi za wakimbizi katikati ya eneo hilo. Shambulizi kubwa lililofanyika juzi liliangusha jengo la ghorofa mbili katikati ya mji wa Deir al-Balah, karibu na Hospitali ya Mashahidi ya Al-Aqsa, na kuwaua watu 20.

Hata hivyo, Rais wa Israel, Isaac Herzog ameitaja kesi hiyo sawa na ukatili na upuuzi.

"Tutafika mahakama ya Kimataifa ya Haki na tutawasilisha kwa fahari utetezi wetu wa kujilinda chini ya sheria za kibinadamu," alisema.

Wakati huo huo, Colombia imekuwa nchi ya kwanza kuunga mkono kesi ya mauaji ya halaiki iliyofunguliwa na Afrika Kusini dhidi ya Israel.

Aidha, Mkuu wa Shirika la Afya Duniani (WHO), Tedros Ghebreyesus ametoa wito kwa nchi ya Israel kuidhinisha maombi ya shirika lake na taasisi zingine ambazo zinataka kupeleka misaada ya kibinadamu kaskazini mwa Gaza.

**DW**

# Samia atunukiwa nishani ya kipekee

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, amewatunuku viongozi mbalimbali nishani ya Mapinduzi huku akimtunuku Rais Samia Suluhu Hassan nishani ya kiongozi mwenye sifa za kipekee.

Utaratibu huo wa utoaji nishani umekuwa ukifanywa na serikali ya Zanzibar kila mwaka siku moja kabla ya kilele cha maadhimisho ya Mapinduzi.

Katika miaka 60 ya Mapinduzi, Rais Samia alitunukiwa nishani hiyo na kuvishwa na Rais Mwinyi katika hafla iliyofanyika jana katika viwanja vya Ikulu Zanzibar.

Mbali na Rais Samia, Dk. Mwinyi aliwatunukia na kuwavisha nishani ya Mapinduzi viongozi na wananchi wenye sifa maalum akiwemo aliyekuwa Waziri Kiongozi na baadaye Makamu wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar, Hayati Maalim Seif Sharif Hamad.

Wengine waliotunukiwa nishani ni Makamu wa Rais Mstaafu, Dk. Mohammed Gharib Bilal na Shamsi Vuai Nahodha aliekuwa Waziri Kiongozi wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar (SMZ) na Balozi Seif Ali Iddi aliyekuwa Makamu wa Pili wa Rais Zanzibar.

Waliotunukiwa nishani ya utumishi uliotukuka ni Dk. Abdulhamid Yahya Mzee aliyekuwa Katibu Mkuu Kiongozi wa SMZ, Prof. Saleh Idris Muhammed na Salum Faki Hamad.

Dk. Mwinyi pia aliwatunuku nishani ya utumishi wa muda mrefu na utii kwa Idara Maalum za SMZ Mohammed Suleiman Haji, Maryam Kurwa Nassor, Seif Omar Makwega na Khadija Ahmada Rai.

Waliotunukiwa nishani ya ushujaa ni marehemu Ramadhan Khalfan Ngozoma, Ikrab Mikidadi Hassan, marehemu Khalid Abss Hassan na Suleiman Maulid Mussa.

Akisoma wasifu wa Rais Samia, Meja Martin Mabena kutoka Jeshi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ) alisema Dk. Samia ni kiongozi wa kwanza mwanamke kushika nafasi ya juu ya uongozi wa nchi ambaye alishika nafasi ya Makamu wa Rais wa Tanzania na baadaye Rais wa Tanzania.

Alisema, Dk. Samia ni kiongozi wa mfano aliyefanya kazi kuanzia ngazi ya chini ya mtunza kumbukumbu (masjala) lakini pia alikuwa Waziri wa Wanawake na Watoto, Waziri wa Utalii, Biashara na Uwekezaji katika SMZ.

Alisem, Rais Samia pia alikuwa Waziri katika serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania akiwa Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano.

Meja Mabena alisema alipokuwa Waziri wa Utalii, alijenga misingi imara ya kukuza biashara ya utalii wakati awali uchumi wa Zanzibar ulikuwa ukitegemea karafuu zao ambalo lilishindwa kufanya vizuri kwa wakati huo.

Alisema Dk. Samia kupitia biashara ya utalii alifanikiwa kuitangaza Zanzibar na Tanzania kimataifa na kuongeza kasi ya ukuaji wa utalii wa ndani na hadi sasa anaendelea na jitihada hizo kupitia filamu ya Royal Tour.

Alisema, Dk. Samia amefanya kazi katika serikali zote mbili kwa uzalendo na utii wa hali ya juu na kuhakikisha Tanzania inapata maendeleo makubwa ya kiuchumi na kijamii.

Pia alisema Dk. Samia amethubutu kulinda na kudumisha Mapinduzi ya Zanzibar ya mwaka 1964 na kuhakikisha Zanzibar na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika hali ya ulinzi na kuimarisha amani, utulivu na mshikamano bila ya ubaguzi wa rangi siasa, dini, jinsia wala ukabila kama ilivyo adhama ya Mapinduzi ya Zanzibar.


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA HAKIMU MKAZI**
**KIVUKONI/KINONDONI**

**SHAURI LA MADAI NO. 25552 YA 2023**

**BANK OF AFRICA TANZANIA LTD........MDAI**

**VERSUS**

**JUDITH BRYSON MASACKY.......MDAIWA**

**Kwa: JUDITH BRYSON MASACKY – DAR ES SALAAM**

Kwa kuwa mwombaji ameleta maombi ambayo maelekezo ya maombi yameelezwa katika nakala za maombi ambazo zinaweza kupatikana katika Mahakama hii, kwa hiyo unatakiwa kuhudhuria katika Mahakama hii ya Wilaya binafsi au Wakili au Mwakilishi ambaye anayeruhusiwa kabla au siku ya tarehe 5 Mwezi wa 2 Mwaka 2024 saa mbili (2:00) kamili asubuhi. Kwa kuwa siku hiyo ni kukatwa kwa shauri unatakiwa kuja na vielelezo vyote vinavyohusiana na maombi haya.
Hati hii imetolewa kwa amri yangu na Chapa ya Mahakama leo tarehe 10 Mwezi wa 1 Mwaka 2014.

HAKIMU MKAZI
MAHAKAMA YA KINONDONI/KIVUKONI

**PETROL STATION FOR "LEASE"**
**10/01/2024**

1. LAKE MIANZINI -PLOT NO 160
2. LAKE HIMO-PLOT NO13

OFFER STANDS FOR 15 DAYS

APPLY TO THE FOLLOWING ADDRESS POST BOX 8405 MOSHI AND VIA

EMAIL
jobsvoluntary@gmail.com

**KUPOTEA KWA CHETI**



**JUMA HASHIM JUMA,** Anatangaza kupotea kwa cheti cha Chuo chenye **No BA. (ED) 00006724** kilichotolewa na Chuo Kikuu cha Dodoma Mwaka 2018. Yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi.
TAARIFA YA POLISI: **PHQ/DOD/DOD/1069/2024**

**KUPOTEA KWA KADI YA GARI**

**LEYLA JOHN MBWAMBO** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T 681 DZP** aina ya **NISSAN DUALS.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi kilichopo karibu.
Taarifa ya Polisi: **PHQ/DAR/TEM/4367/2024.**

**KUPOTEA KWA KADI YA GARI**

**MATABA MBOJE MWAGALA** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari yenye usajili namba **T 690 CJS.** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi .
POLISI TAARIFA: **PHQ/TAN/MUH/3850/2023**

**KUPOTEA KWA KADI YA GARI**

Ndugu **MUKUTASIDU MUDRIKATI MWESIGE** anatangaza kupotelewa na kadi yake ya gari aina ya MITSUBISH FIGHTER lenye namba za usajili T344 DUR injini namba 6D17724835 na chassis namba FK618K500311. Ametoa taarifa polisi na kupewa namba **PHQ/KAG/KYE/313/2024,** Yeyote atakayeiona atoe taarifa polisi au awasiliane naye kwa namba 0789888981.

MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

## Mapinduzi yameleta manufaa makubwa, yalindwe na kuenziwa

**WANANCHI** wa Tanzania leo wanaadhimisha miaka 60 ya Mapinduzi ya Zanzibar ambayo yaliung'oa utawala dhalimu wa Sultan uliokuwa akiwakandamiza wazawa na kuonekana watwana ndani ya ardhi yao.

Katika mapinduzi hayo matukufu yaliyofanyika mwaka 1964, Wazanzibari wanyonge ambao wengi walikuwa wakulima, wakwezi na wavuvi, wakiongozwa na chama cha Afro Shiraz (ASP) chini ya Sheikh Abeid Amani Karume, walifikia kikomo cha uvumilivu na kusema inatosha, hivyo wakati wa kujikomboa ulikuwa umewadia. Chini ya utawala wa Sultani, Wazanzibar hawakuwa na nafasi ya kumiliki ardhi na huduma nyingi za muhimu kama elimu na afya hawakuzipata.

Baada ya Mapinduzi hayo, Serikali ya Mapinduzi Zanzibar chini ya Rais wa kwanza, Hayati Karume, ilitangaza rasmi kwamba matibabu na elimu kwa wananchi wote ni bure na Wazanzibari wanaruhusiwa kumiliki ardhi. Hatua hiyo ilisababisha baadhi ya wananchi kupewa ardhi kwa ajili ya matumizi ya shughuli za uzalishaji.

Pia ubaguzi wa rangi kwa misingi ya watu wa asili ya kiasia waliokuwa wengi wakati huo na Waafrika ulifutwa rasmi na wakaanza kuoana. Watu wote waliishi kwa usawa bila kujali dini, rangi wala maeneo wanayotoka, hivyo ndivyo ikawa Zanzibar mpya.

Kutokana na Zanzibar kujikomboa kwa njia ya Mapinduzi hayo matukufu, jitihada za kuwainua wananchi kutoka katika umaskini uliotopea zilianza kwa serikali kuanza kujenga miundombinu mbalimbali yakiwamo majengo ya makazi kama vile magorofa ya Michenzani, Unguja na kuwawezesha wananchi kuishi katika mazingira bora.

Tangu uongozi wa Sheikh Karume mpaka sasa wa Dk. Hussein Ali Mwinyi, ni awamu nane sasa zimefika na kila awamu ilijitahidi kuhakikisha inakuza uchumi na ustawi wa wananchi. Kutokana na azma ya uongozi, kila awamu ilishuhudia mabadiliko makubwa ya kisiasa, kiuchumi na kijamii ndani ya visiwa hivyo.

Tofauti na ilivyokuwa kabla ya muda mfupi baada ya Mapinduzi yako mageuzi makubwa katika sekta mbalimbali kama vile elimu, afya, miundombinu na uwekezaji katika miradi ya kiuchumi ambayo imeifanya Zanzibar kuwa sehemu ya mfano ndani ya Afrika na duniani kwa ujumla.

Shule na hospitali kwa mfano, zilikuwa chache kulinganisha na sasa jambo ambalo halikutoa nafasi kwa wananchi wote kupata fursa katika huduma hizo. Lakini kwa sasa kuna taasisi za elimu kuanzia shule za awali, msingi sekondari mpaka vyuo vikuu, ambazo zimewezesha Wazanzibar wengi kupata elimu na sasa kuna wasomi ambao wanatumika ipasavyo katika nafasi mbalimbali serikalini.

Katika afya pia kulikuwa na vituo vya huduma vichache lakini ndani ya miaka 60 zinapatikana kuanzia zahanati, hospitali za wilaya, mikoa,rufani mpaka hospitali kuu ambazo zinatoa matibabu huku zikiwa zimesheheni huduma kama maabara, matibabu ya kibingwa na dawa za kutosha.

Miundombinu ya usafiri na usafirishaji imeimarishwa mwaka hadi mwaka na serikali ya sasa imeongeza kasi katika eneo hilo. Hivi sasa kuna kasi ya ujenzi wa bandari, viwanja vya ndege Zanzibar na Pemba na barabara kila kona ya Zanzibar. Hali hiyo imesaidia kurahisisha usafirishaji wa abiria na mizigo ndani na nje ya nchi.

Hali ya utulivu na usalama pamoja na utulivu wa kisiasa imechangia pia kuwapo kwa kasi ya uwekezaji visiwani humo. Hoteli nyingi zimejengwa ndani ya Zanzibar na watalii wamekuwa wakiongezeka mwaka hadi mwaka na kuchangia kwa kiasi kikubwa pato la taifa. Hayo ni machache lakini kuna mengi ya kujivunia ndani ya miaka 60 ya Mapinduzi.

Kwa jumla, Mapinduzi matukufu ya Zanzibar yameleta neema kubwa kwa wananchi hasa katika maendeleo ya kijamii na kiuchumi. Zote hizo ni jitihada za viongozi toka Mapinduzi mpaka sasa kutokana na maono waliyokuwa nayo. Ni vyema Mapinduzi haya yakaenziwa na kulindwa kwa ustawi wa Wazanzibari na Watanzania kwa ujumla.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Dennis Ntaita, 0713 578 284
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677 020 701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Adam Fungamwango

# Kilichovunwa Mapinduzi Matukufu Zanzibar, jamani hesabu si haba!

**ULIKUWA** usiku wa kuamkia leo, lakini tofauti ni miaka 60 sasa imepita, wananchi wa hali ya chini Zanzibar walipochoka dhuluma, kupuuzwa, kuonewa na kunyanyaswa, wakaamua kumuondoa Sultani wa Zanzibar na serikali yake, iliyoundwa na Waarabu chini ya Wakoloni.

Wananchi ambao wengi walikuwa ni wakwezi, wakulima, na wavuvi, wakaamua 'liwalo na lile' kwa marungu na silaha za jadi, kwa umoja wao wakapambana na kumuondoa Sultani huyo.

Usultani wa Zanzibar ulikuwa umepewa dhamana na Uingereza, uhuru wa mwaka 1963, lakini mwaka mmoja baadaye Wazanzibari wakaona 'isiwe tabu' kwani bado walionekana hawapati heshima yoyote, wala kipaumbele kwenye mambo mbalimbali ya kijamii kama elimu, afya na hata kubaguliwa.

Baada ya kufanyika mapinduzi hayo, uongozi ukabaki kwa Wazanzibari wenyewe waliokuwa wanapuuzwa na kuonewa. Wenye nchi wakaachiwa nchi yao.

Chini ya chama Afro Shirazi, ikamchagua msuka mipango mkuu wa Mapinduzi Matukufu, Sheikh Abeid Amani Karume kuwa Rais wa Kwanza ya Zanzibar.

Muda mfupi tu, wakateta na maswahiba wao wa Tangayika walioshirikiana kwa shida na raha, kukashuhudiwa Muungano wenye sura ya kipekee duniani, mwaka huohuo 1964 kukaundwa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Awali, wale waliokuwa wakakubaliana na mapinduzi hayo walidhani kwamba uongozi utashindwa.

Nchi itawashinda Wanzanzibar ili wapate la kusema kuwa utawala ungebaki kwa Waarabu, lakini kadri miaka inavyozidi kwenda midomo yao ikafunga.

Wanachokiona leo waliopo hao hawaamini na wapo ambao baada ya kuona maendeleo yanapatikana, wakawa na kazi ya kufanya hujuma, ili mradi tu ionekana hakuna chochote kinachofanyika wapate cha kuongea, lakini wapi.

Uongozi ukakaa imara na kila Rais aliyeingia madarakani, akaendelea kuyaenzi mapinduzi yao na kuweka mifumo ya maendeleo, huku aking'oa matabaka yote ya zamnai na mapya

Chama cha Afro Shirazi, ambayo baadaye ikaungana na TANU mwaka 1977 na kuunda Chama Cha Mapinduzi (CCM), kimeendelea kubaki kikitoa mapendekezo na maelekezo kadhaa kwa serikali yake, kwa ajili ya kuangalia na kutatua kero za muungano.

Tukirudi kwenye faida za Muungano, ni kwamba awali huduma zilitokana kwa ufinyu, hasa kwa kinamama na Watoto, hawakupata matibabu ya uhakika kiasi cha kusababisha vifo visivyotarajia.

Kwa sasa Zanzibar ina hospitali zinazohudumia watu wote bila ubaguzi au kulipa kisasi cha kile kilichotokea kabla ya Mapinduzi. Hiyo pia , ipo katika elimu, Wazanzibari wengi wamesomeshwa na serikali yao ndani na nje ya nchi. Hadi sasa kuna kundi la waliorejea nyumbani kuilipa nchi faida

Leo hii, Zanzibar ina utajiri wa viwanda vingi na bora, tofauti na ilivyokuwa wakati wa utawala wa Kisultani, hivyo kuwapa ajira watu wengi, vilevile ajira hizo hazichagui mtu, eneo alilotoka wala tabaka, ili mradi tu awe na uwezo wa kuifanya kazi hiyo na vigezo vyake.


Tunatoa pongezi kubwa na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar (SMZ), ambayo kwa sasa ipo chini ya Rais Dk. Hussein Ali Mwinyi, kwani ameonekana kuendeleza pale ambako marais wenzake waliishia.

Penye michezo, ni kwamba hivi karibuni tumeona marekebisho makubwa ya Uwanja wa Aman, Unguja ambao ulijengwa kipindi cha awamu ya kwanza ya utawala.

Faida nyingine ni kwamba ,Zanzibar kwa sasa imekuwa ikitoa vipaji vingi vya wachezaji ambao wamekuwa na faida kwa taifa lote la Tanzania.

Hizi ni faida chache tu na matunda yaliyopatikana kutokana na Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar ambayo leo yanatimiza miaka 60.

# MIAKA 60 MAPINDUZI ZANZIBAR



Abeid Amani Karume



Dk Hussein Ali Mwinyi



Aboud Jumbe Mwinyi




Dk. Ali Mohamed Shein



Ali Hassan Mwinyi



Amani Abeid Karume



Idris Abduwakil



Salmin Amour

# Uchumi wa Buluu unavyoipaisha Zanzibar kimaendeleo

Na Mwandishi Wetu

RAIS Dk. Hussein Ali Mwinyi baada ya kuingia madarakani Zanzibar Novemba, 2020 katika kutangaza Baraza la Mawaziri, aliunda wizara mpya ya Uvuvi na Uchumi wa Buluu. Lengo kubwa la kuanzishwa kwa wizara hiyo lilikuwa kuharakisha maendeleo endelevu ya wananchi wa Zanzibar na kuongeza pato la taifa kupitia rasilimali za bahari.

Dhana kubwa ya kuwapo kwa falsafa hiyo ambayo imedumu kwa zaidi ya miaka mitatu ilikuwa kuleta mageuzi ya kweli ya maendeleo ya kiuchumi na kijamii ikizingatiwa kwamba Zanzibar ilivyozungukwa na bahari na rasilimali nyingi ambazo zina nafasi kubwa ya kuupaisha uchumi wake na Tanzania kwa ujumla.

Miongoni mwa maeneo yaliyoainishwa katika utekelezaji wa uchumi wa buluu ni maendeleo ya uvuvi na mazao ya bahari, utafutaji wa mafuta na gesi, usimamizi wa rasilimali na mikataba ya sayansi na teknolojia, utafiti na ubunifu wa kiuchumi na maeneo mtambuka, uhifadhi wa mazingira na rasilimali za bahari.

Katika kuhakikisha yote hayo yanafanikiwa, Katibu Mkuu wa Wizara ya Uvuvi na Uchumi wa Buluu, Dk. Aboud Suleiman Jumbe, anasema taasisi na idara ziliundwa na kuimarishwa (kwa zile zilizokuwapo). Miongoni mwa idara na taasisi hizo ni Idara ya Maendeleo ya Uratibu wa Uchumi wa Buluu, Idara ya Maendeleo ya Uvuvi, Shirika la Uvuvi Zanzibar (ZAFICO), Mamlaka ya Usimaizi na Ufuatiliaji Mafuta (ZPRA) na Shirika la Maendeleo ya Petroli Zanzibar (ZPDC).

"Idara ya Maendeleo na Uratibu wa Uchumi wa Buluu inaunganisha taasisi za utalii na kama wizara tunashirikiana na Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale kwa ajili ya usafiri wa baharini, bandari, biashara, miundombinu na mnyororo wa thamani.



Dk. Aboud Suleiman Jumbe

Pia tunashirikiana na Wizara ya Maji, Nishati na Madini kutokana na dalili kubwa kwamba tunaweza kuanza na gesi kutokana na bonde la bahari lililopo. Pia masuala ya umeme wa upepo na jua," anasema Dk. Aboud.

Suala lingine linalozingatiwa katika maendeleo ya uchumi wa buluu, kwa mujibu wa Dk. Aboud, ni utawala bora wa bahari kwa maana ya hifadhi ya mazingira, mabadiliko ya tabianchi, na usalama wa mipaka ya bahari.

Anasema ili kufikia azma hiyo, viliwekwa vipaumbele kama vile kutoa elimu ya uelewa na ufahamu kwa wananchi walioko kando ya madini chumvi; ubunifu kuhusu vipaumbele katika uchumi wa buluu ili kuona wananchi wananufaika vipi katika uvuvi na mazao ya bahari, ajira, utalii na sekta mpya zitakazojitokeza na ushirikishaji wa wadau na sekta binafsi.

"Kipaumbele kingine kilikuwa zana. Wananchi wapate zana bora kwa njia ya mkopo, ufadhili na mikopo nafuu na wengi wamechangamkia benki haraka baada ya kuwapo mwitikio wa benki kupitia dhamana za serikali zote mbili (Muungano ya Zanzibar).

"Pia mkazo uliwekwa kwa wafugaji wa matango bahari na wafugaji wa samaki kupata manufaa, ajira na ujasiriamali. Mikopo ilikuwa kipaumbeke cha nne kupitia fedha za Uviko- 19, benki mbalimbali, BBT kama Benki ya Uwekezaji Ulaya (EIB), Exim na Benki ya Watu wa Zanzibar (PBZ)," anasema.

Suala lingine la kipaumbele, kwa mujibu wa Dk. Aboud ni masoko kwa maana ya wazalishaji kupata masoko ya uhakika ya ndani na nje kama Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo (DRC) na Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC), China na Korea Kusini

**MATOKEO CHANYA**

Tangu kuanza kwa utekelezaji huo, kumekuwa na matokeo chanya ndani ya miaka mitatu ikiwamo kuongezeka kwa uwekezaji na mazao yanayopatikana kupitia shughuli mbalimbali. Dk. Aboud anasema licha ya sekta nyingi kushambuliwa na Uviko- 19 ikiwamo uchumi wa buluu kumekuwa na mafanikio makubwa ndani ya miaka mitatu.

"Kupitia mikakati na utekelezaji wa

Inaendelea uk. 9

WIZARA YA UCHUMI WA BULUU NA UVUVI ZANZIBAR

MIAKA 60

YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR

1964 - 2024

Menejimenti na Wafanyakazi wote wa Mamlaka ya Kusimamia Uvuvi wa Bahari Kuu tunaungana na Mh. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dkt. Hussein Ally Hassan Mwinyi pamoja na Wananchi wote kwa ujumla katika kuadhimisha Miaka 60 ya Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar.

"uchumi wa bluu kwa uvuvi endelevu. "



Mh Dk Hussein Ali Mwinyi
Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi

MAWASILIANO
Zura Building, Ground Floor Maisara, Zanzibar
Simu: +255 24 2941195 / +255 24 2941197, Barua Pepe: info@blueeconomysmz.go.tz

# Uchumi wa Buluu unavyoipaisha Zanzibar kimaendeleo

**Inatoka uk. 8**

wa uchumi wa buluu, uvuvi wa samaki umepanda kutoka tani 38,000 hadi 80,000 sasa na mwani kutoka tani 8,000 hadi 14,000. Matango bahari mwaka 2019 yalivunwa tani 30 kwa mwaka lakini kutokana Uviko- 19 uzalishaji ulishuka hadi tani 5.58 lakini kupitia ahueni za Uviko- 19 yaliongzeka hadi tani 15 hadi 20 kwa mwaka na sasa umepaa hadi tani 45 kwa mwaka," anabainisha.

Kuhusu kaa, anasema mwaka 2019 mavuno yalikuwa zaidi ya tani 100 lakini kutokana na Uviko- 19 yalishuka hadi tani 30 lakini sasa yamepanda hadi kufikia tani 175 kwa mwaka.

"Hali hiyo pia imetokana na kuwapo kwa mashamba ya kaa 30 Unguja na 30 Pemba na uvunaji utakapoanza uzalishaji unaweza kufikia tani 300 kwa mwaka. Hii itaboresha hali ya maisha ya Watanzania," anasema.

Mafanikio mengine yaliyopatikana kupitia uchumi wa buluu ni ukombozi wa wanawake kiuchumi. Wanawake wengi wamejitokeza na kushiriki kikamilifu katika kilimo cha mwani, hivyo kuwainua kiuchumi tofauti na ilivyokuwa awali.

**UVUVI BAHARI KUU**

Sekta ya uvuvi wa bahari kuu, kwa mujibu wa Katibu Mkuu, ina lengo la kuipeleka Tanzania katika kesho imara. Anasema ndani ya miaka mitatu ya uongozi wa Rais Dk. Mwinyi, kumekuwa na maendeleo makubwa katika eneo hilo.

Dk. Aboud anasema wakati Dk. Mwinyi anaingia madarakani kulikuwa na meli tatu zilizokuwa zikifanya shughuli hiyo lakini baada ya juhudi kubwa, hivi sasa kuna zaidi ya leseni 100 za uvuvi wa bahari kuu.

Leseni moja ina maanisha meli moja ya uvuvi, kwa maana hiyo kuna zaidi ya meli 100 za uvuvi katika bahari kuu. Hatua hiyo, anasema imefungua mipaka na vivutio kwa wawekezaji katika uvuvi wa jodari.

Pia anasema mpango huo umeongeza wigo wa uwekezaji katika viwanda vya kusarifu dagaa Manga Pwani na Kilwa pamoja na uchakataji wa jodari. Hatua hiyo, anasema pia imetengeneza ajira kwa wananchi.

"Tanzania ni mwanachama wa Umoja wa Mataifa (UN) na imeingia mikataba mbalimbali ya kimataifa kuhusu bahari na inatekeleza lengo namba 14 la Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDG). Hii pia imesaidia kuimarisha mapambano dhidi ya mabadiliko ya tabia nchi, usalama wa bahari, biashara za magendo na dawa za kulevya," anabainisha.

**FALSAFA YA MAPINDUZI**

Wakati Zanzibar leo inaadhimisha miaka 60 ya Mapinduzi, Dk. Aboud anasema Uchumi wa Buluu unaendana na falsafa ya Mapinduzi Matukufu ya mwaka 1964. Anasema lengo la Mapinduzi lilikuwa kuwakomboa wananchi kutoka kwenye utawala uliowafanya wawe wanyonge ndani ya ardhi yao na wasiwe na sauti.

Anasema uwezeshaji ilikuwa ajenda kuu ya Mapinduzi kwa maana ya kumkwamua mwananchi katika hali ya unyonge na hiyo inajidhihirisha katika mipango mbalimbali iliyoanzishwa na SMZ kwa nyakato tofauti kama vile MTAKULA, Mpango wa Kukuza Uchumi Zanzibar (MKUZA) na Mpango wa Maendeleo Zanzibar (ZADEP).

"Malengo ya mipango hii yote ni kumwezesha mwananchi kiuchumi. Hata falsafa ya Uchumi wa Buluu inashabihiana na mipango iliyotangulia ambayo lengo lake lilikuwa uwezeshaji wa wananchi bora za maisha.

"Maana halisi ya falsafa hii ni kwamba mwananchi atakaposhirikishwa, atakuwa na uwezo wa kutambua nafasi yake na kushiriki kikamilifu katika ulinzi na usalama wa rasilimali zake. Hivi ndivyo ilivyo na wananchi wanashiriki katika ulinzi wa rasilimali kwa kuwa wanatambua ni kitu muhimu kwa maisha yao na maendeleo yao kwa ujumla," anasisitiza.

Anasema katika kufanikisha azma hiyo, serikali imetengeneza mfumo jumuishi katika usimamizi wa rasilimali kwa kuwapa wananchi elimu, nyenzo na fursa ili kuwa walinzi wa rasilimali za bahari.

Hali hiyo, anasema ni tofauti na Zanzibar ilipokuwa chini ya wakoloni ambao lengo lao lilikuwa kujinufaisha na rasilimali hizo na kuwaacha wananchi wakiendelea kuwa maskini.

"Utafiti unaonyesha kwamba wakati wa utawala wa mwanzo wa Sultani mwaka 1840, usimamizi wa rasilimali ulikuwa na lengo la kudhibiti uvunaji wa mikoko na ilivunwa kwa ajili ya kwenda kujenga merikebu na majahazi. Hata Waingereza walipochukua Zanzibar na Pwani, walitengeneza sheria za usimamizi wa rasilimali kwa manufaa yake. Kwa hiyo watawala walifanya hivyo kwa manufaa yao na si wananchi," anasema.

Ndani ya muda mfupi, uchumi wa buluu umeonyesha mafanikio makubwa kwa maendeleo ya Zanzibar na wananchi kwa ujumla. Hali hiyo inatoa picha kwamba mipango na mikakati imara, kama ilivyo sasa, itaipeleka Zanzibar na Tanzania kwa ujumla katika viwango vya juu katika maendeleo ya kiuchumi na kijamii.

SERIKALI YA MAPINDUZI ZANZIBAR
WIZARA YA MAJI NISHATI NA MADINI

Maadhimisho ya Miaka 60 ya Mapinduzi
1964 - 2024

Uongozi na Wafanyakazi wa Wizara ya Maji, Nishati na Madini wanatoa Pongezi kwa Raisi wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Hussein Ali Mwinyi pamoja na wananchi wote wa Zanzibar kwa kuadhimisha miaka 60 ya Mapinduzi ya Zanzibar.



Mh. Dr.Hussein Ali Mwinyi
Rais wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar

MUNGU IBARIKI ZANZIBAR

MIAKA 60 YA MAPINDUZI

# Undani wa kilimo karafuu Z'bar na alichokinadi Dk. Samia Pemba

Na Peter Orwa

WAKATI akiwa kwenye uongozi, Rais Dk. Ali Mohamed, alionekana katika sura kuu mbili za kiutawala, ndani ya Zanzibar kuhusu kilimo cha zao la karafuu.

Kutoka sura moja akipigana kuipa thamani karafuu na mkulima wake shambani, upande wa pili akahimiza ibaki zao la Mzanzibari, kuanzia uzalishaji shambani, hadi mfumo wa mauzo yake nje ya nchi.

Eneo mojawapo alikoelekeza nguvu za mapambano Rais wa Zanzibar Dk. Ali Mohammed Shein, ni kwenye kuilinda bidhaa hiyo, dhidi ya uchepushaji kwenye soko bubu la nchi jirani, ikivuka bahari kutumia mitumbwi na maboti.

Ndani ya nyayo hizo, Jumanne wiki hii Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, ambaye ana historia ya kutumikia Baraza la Mawaziri na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, akarudia tena hoja hiyo akitetea uzalishaji wa karafuu, ulisuasua katika miaka ya kati, Zanzibar.

Ilikuwa katika hafla ya kuzindua jengo la Shirika la Biashara Zanzibar (ZSTC), huko Pemba wiki hii, Dk. Samia akataja, dhamira iliyopo sasa ni kuongeza thamani ya karafuu Zanzibar.

Anasema hiyo inaendana na kuwekezwa viwanda binafsi vya kuchakata mavuno hayo, viwili vikiwa njiani huko Pemba, ambako kuna tija kubwa shambani.

Anasema kati ya miaka ya 1960 hadi 1978 uzalishaji ulikuwa juu kufikia tani 20,000 baadaye ukashuka sana, chini ya tani 10,000, ila juhudi zinafanyika kukiwapo malengo kukuza uzalishaji kufikia tani 10,000.

Kuhusu bei, Rais Dk. Samia anataja kuwapo tija katika kiwango cha uzalishaji shambani na mabadiliko ya bei ya ununuzi yanapanda kwa mkulima, kutoka Sh. 3,500 hadi Sh. 3,800 kwa kilo.

Rais anasisitiza kwamba bado soko lipo na uzalishaji haujafikia kiwango kinachohitajika sokoni, vilevile tija ya shambani haijafikia kiwango kinachotakiwa katika soko la kimataifa.

Kupitia wigo wa Diplomasia Uchumi, anasema balozi za nchini zimekuwa zikihimizwa kufuatilia na kupanua wigo wa soko na akashauri kuwapo hoja ya uwekezaji katika mashamba ya serikali.

Hadi sasa zao la karafuu, bidhaa ya kihistoria, ndio inasadiana na mbia wake, Sekta ya Utalii katika kukuza uchumi wa Zanzibar.

**KARAFUU ILIVYOLETWA**

Kimsingi, karafuu ni zao linalotokana na mmea mkarafuu. Ingawa haimo katika kundi la vyakula wala vinywaji, lakini ni kiungo muhimu sana.

Yanatajwa matumizi yake yanajumuisha kutengeneza sigara, upishi, aina za dawa za meno, pia mafuta yake hutumika kuchua misuli.

Kurejea maandiko ya kihistoria, mikarafuu ilianza kupandwa kwenye visiwa vya Shelisheli, Mauritius na



RAIS Dk.Hussein Ali Mwinyi, akishiriki kazi ya uchambuaji karafuu katika kambi ya Said Salim Ali (kulia kwa Rais) na kushoto kwake ni Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini Pemba, Salama Mbarouk Khatib. **PICHA ZOTE: MTANDAO.**

> **"Ingawa kuna maeneo ya serikali, maeneo yanayomilikiwa na serikali ambayo yana karafuu na serikali inawakodisha watu ambao wanataka kukodi, kuchuma na kuuza, mashamba hayo yapo Zanzibar na Pemba."**

sehemu nyinginezo. Miche yake ikaletwa Zanzibar kutoka Mauritius mwaka 1818. Mito hiyo ikastawi zaidi Unguja na Pemba, ambako inatoa asilimia 80 ya karafuu zinazohitajika duniani, hata kufanya uchumi wa Zanzibar kutegemea sana zao hilo.

Ufafanuzi wa Shirika la Biashara la Taifa Zanzibar (ZSTC), ni kwamba karafuu ina historia ndefu ambayo ofisa wake, Suleiman Juma Jongo, anaeleza kwamba:

"Miche ya mikarafuu kuja kwake hapa (Zanzibar) imetokana na visiwa vya Indonesia, Mashariki ya mbali. Ilifika huko Madagascar na Shelisheli katika karne ya 19, ndiyo ikaja hapa kwetu Zanzibar na kupandwa, wakati wafalme wa Oman walipotawala hapa.

"Kimbunga kiliwahi kutokea na kiling'oa mikarafuu mingi. Kwa hivyo, kukawa na juhudi mpya ya wafalme wa wakati ule ya kupanda mikarafuu mipya.

"Ilikuwa si kitu cha hiari, bali ililikuwa ni jambo la lazima, watu wapande mikarafuu kwa sababu kitu hicho kinasaidia uchumi. Kabla ya Mapinduzi, mashamba ya mikarafuu yalikuwa ya watu binafsi, lakini baada ya Mapinduzi (1964), serikali ilitaifisha ardhi na kuigawa kwa wananchi.

"Kila mwananchi alipata heka tatu za kumwezesha kulima, kupata chakula chake, na kupata mahitaji yake ili ajiendeleze na familia yake. Hali hiyo imeendelea mpaka leo.

"Sasa suala la karafuu linamilikiwa na wananchi wenyewe. Idadi kubwa ya mashamba yalikuwapo ya wananchi wenyewe.

"Ingawa kuna maeneo ya serikali, maeneo yanayomilikiwa na serikali ambayo yana karafuu na serikali inawakodisha watu ambao wanataka kukodi, kuchuma na kuuza, mashamba hayo yapo Zanzibar na Pemba."

Jongo anaendelea: "Sasa utaratibu wa upandaji zao la karafuu, bado unashughulikiwa na Wizara ya Kilimo (Zanzibar), Wizara ya Kilimo, ndiyo yenye idara maalum ya kuendeleza mazao haya ya biashara. Sasa, Wizara ya Kilimo ndiyo inashughulika kuwa na vitalu vya miche ya karafuu."

"Kwa kuwa ZSTC ndiyo inayoshughulikia zao la karafuu, serikali kupitia Wizara ya Biashara ya ZSTC, inachangia maendeleo ya zao la karafuu," anatamka Jongo na kuendelea kufafanua majukumu hayo:

" Inawalipa vibarua wanaoshughulikia kuendeleza upandaji wa mikarafuu mipya katika sehemu mbalimbali ambazo mikarafuu imekufa, ZSTC inanunua zana za kutengeneza miche na kupanda miche mpaka kuisambaza kwa wananchi."

**MWANZO WA MASHAMBA**

Mosese Hatibu, ni mtaalamu katika taasisi ya Utafiti wa Kilimo Zanzibar - Unguja, anayeelezea mikarafuu inavyooteshwa miche ya karafuu na jinsi ya kuitunza.

"Kwanza, unatayarisha eneo lako, unapiga tuta, kisha unaweka mbolea, halafu unachukua majani makavu yaliyotokea katika mikarafuu. Unapiga mistari unaweka zile mbegu za mikarafuu ambayo ni matende.

"Ukishapanda, unafunika majani makavu ya mkarafuu, unamwagilia maji halafu unaweka kivuli, unapalilia kila baada ya wiki. Baada ya mwezi mmoja, matende tayari yashaanza kuchipua, unaiacha miche yako vile mpaka itimie miezi miwili.

"Baada ya miezi miwili, unaenda kung'oa unachukua kimoja kimoja pamoja na kile kitende chake, kile ambacho ni mchele mkarafuu uliochipua unauchukua na kuuweka kwenye mifuko," anasema.

"Mifuko hiyo inakuwa imewekwa udongo ambao umechanganya na mbolea, halafu unachukua "humus" ambayo ni takataka zenye mbolea, una mchanganyiko huu unaweka kwenye mifuko."

"Unapandikiza miche yako, unaitunza inakaa kwa muda wa miezi mitatu mpaka minne. Miche yako imeshakuwa tayari, imeshakuwa mikubwa ina majani sita mpaka manane unaiacha kwa miezi sita. Baada ya miezi sita miche yako inakuwa tayari kwa kupelekwa shambani.

"Katika msimu wa mvua wa masika au vuli, unakwenda kupiga mashimo unapanda, sasa katika kupanda shambani mikarafuu mimi nashauri wakulima wapande na mazao mengine na ili shamba la mikarafuu liwe safi, wapande mihogo au migomba ili kupata kivuli na shamba liwe safi sio wapande mikarafuu mitupu."



Mkulima akihudumia mkarafuu wake shambani, Pemba.



Majengo ya shule za ghorofa ya Shule ya Tumekuja iliyoko Unguja na shule ya Maziwang'ombe iliyoko Pemba.

# Maendeleo makubwa ya elimu miaka 60 Mapinduzi

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

ELIMU ni msingi mkuu wa maendeleo ya kijamii na kiuchumi. Kwa kutambua hilo, mara baada ya Mapinduzi Matukufu ya mwaka 1964, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar (SMZ) chini ya Sheikh Abeid Amani karume, ilitangaza kuwa elimu kwa wananchi wote itatolewa bure.

Sera hiyo inaendelea hadi sasa Zanzibar ikiwa imetimiza miaka 60 huku watu wote, wakipata huduma hiyo bure. Mapinduzi ya mwaka 1964, ndiyo siri ya maendeleo na Zanzibar imepiga hatua kubwa katika kuwaletea wananchi wote maendeleo bila ubaguzi wa aina yoyote.

Kabla ya Mapinduzi, hakukuwa na fursa sawa katika upatikanaji wa huduma za kijamii, elimu ikiwamo. Shule zilikuwa chache na elimu ilikuwa ikitolewa kwa misingi ya kibaguzi kutegemea na matabaka ya watu.

Jamii kubwa ya Wazanzibari na watoto kutoka familia za kinyonge, wengi wao hawakuwa na fursa ya kupata elimu na waliobahatika walisoma shule zenye hadhi za chini kabisa.

Hali ya ubaguzi iliendelea mpaka Januari 12, 1964 ndipo Wazanzibari waliposhikamana na kuamua kuuondoa udhalilishaji na madhila waliyokuwa wakifanyiwa na utawala wa kikoloni.

Wazanzibari walipambana kumwondoa mkoloni kwa kufanya Mapinduzi ambayo leo hii wanajivunia kutimiza miaka 60 kwa kupiga hatua mbalimbali za maendeleo.

Baada ya kushika hatamu Septemba 23, 1964 SMZ ilitangaza elimu bure ili kutoa fursa sawa kwa wananchi wake kupata elimu bila kujali rangi, kabila, dini, eneo wanalotoka au jinsia.

Azma hiyo ya serikali kuondoa ubaguzi katika elimu, imekuwa ikiendelezwa katika kila awamu ya uongozi. Hayo yanadhihirishwa na hatua kubwa ya maendeleo yaliyofikiwa katika kupanua fursa za upatikanaji wa elimu Unguja na Pemba.

"Kwa sasa tumeimarika zaidi ikilinganishwa na hali ilivyokuwa wakati wa ukoloni. Kabla ya Mapinduzi, Zanzibar ilikuwa na shule moja tu ya maandalizi iliyokuwa na wanafunzi 60 na shule 62 tu za msingi zilizokuwa na wanafunzi 24,334," anasema Katibu Mkuu wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, Khamis Abdallah.

Anasema takwimu za elimu zinaonyesha kuwa hadi mwaka 2023, idadi ya shule zinazotoa elimu ya maandalizi zimefikia 891 zenye jumla ya wanafunzi 102,098 na shule za msingi zimeongezeka na kufikia 649 zikiwa na wanafunzi 380,638.

Kwa shule za sekondari, anasema kabla ya Mapinduzi, kulikuwa na shule tano zenye wanafunzi 1,038 lakini sasa 318 zikiwa na wanfunzi 110,045.

Anasema idadi ya watu Zanzibar kwa kipindi cha miaka 10 iliyopita imeongezeka kutoka 1,303,569 mwaka 2012 hadi 1,889,773 mwaka 2022.

INAENDELEA UK. 13

SERIKALI YA MAPINDUZI ZANZIBAR
WIZARA YA ELIMU NA MAFUNZO YA AMALI

Maadhimisho ya Miaka 60 ya Mapinduzi
1964 - 2024

Uongozi na Wafanyakazi wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali wanatoa Pongezi kwa Raisi wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Hussein Ali Mwinyi pamoja na wananchi wote wa Zanzibar kwa kuadhimisha miaka 60 ya Mapinduzi ya Zanzibar.



Mh. Dr.Hussein Ali Mwinyi
Rais wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar

MUNGU IBARIKI ZANZIBAR

# Mageuzi sekta ya ardhi miaka 60 ya Mapinduzi

**Na Mwandishi Wetu**

ARDHI ni rasilimali muhimu kwa maendeleo endelevu. Bila ardhi hakuna shughuli yoyote ya maendeleo, iwe viwanda, hoteli, viwanja vya michezo, kilimo, ufugaji, ujenzi wa makazi na maeneo ya biashara, miundombinu ya usafirishaji inayoweza kufanyika.

Kutokana na umuhimu huo, ndipo dhana mbalimbali kuhusu upimaji na matumizi bora ya ardhi inapoibuka. Lengo ni kuhakikisha ardhi inatumika ipasavyo kwa maana ya kila shughuli kutengewa eneo mahsusi ili kuepusha mwingiliano wa kisekta na migogoro ambayo inaweza kuathiri usalama na maendeleo kwa ujumla.

Kwa kutambua hilo, katika miaka 60 ya Mapinduzi ya Zanzibar ambayo leo ni kilele chake, Serikali ya Mapinduzi Zanzibar (SMZ) katika kipindi hicho imechukua hatua mbalimbali katika kuhakikisha kunakuwa na matumizi bora ya ardhi.



Katibu Mkuu Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi Dr.Mngereza Mzee Miraji

Kwa maneno mengine, ardhi inapangwa kulingana na matumizi husika na kuleta mandhari mujarabu. Ili kuhakikisha malengo hayo yanatimizwa, wakati Rais wa sasa, Dk. Hussein Ali Mwinyi anaingia madarakani, moja ya mambo aliyoyafanya ni kuleta mageuzi katika sekta ya ardhi kwa kuunda Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi. Awali, sekta hiyo ilikuwa idara katika wizara mbalimbali.

"Wizara hii ilianzishwa mwaka 2020 ikiwa na kurugenzi tatu ambazo ni Makazi (idara mpya), Utumishi na Uendeshaji, na Sera Mipango na Utafiti. Mwanzo, Ardhi ilikuwa chini ya Kamisheni ya Ardhi Zanzibar na makazi ilikuwa chini ya Shirika la Nyumba Zanzibar (ZHC)," anatanabahisha Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Dk. Mngereza Mzee Miraji, alipozungumza na gazeti hili hivi karibuni.

Dk. Mungereza anasema kabla ya Mapinduzi Matukufu ya mwaka 1964, ardhi ilikuwa mali ya serikali ya kikoloni lakini baada ya Zanzibar kujitawala, utekelezaji wa ahadi kuhusu sekta hiyo ulianza kwa SMZ kutangaza kuwa ni mali ya serikali na mwaka 1965 ilitangazwa kuwa wananchi wana haki sawa katika umiliki wa ardhi.

"Mwaka 1965 ekari 26,700 ziligawiwa kwa watu 22,000 maarufu kama 'Eka za Mzee Karume'. Tangu wakati huo hadi sasa kumekuwa na mabadiliko ya sheria na kanuni na watu kumilikishwa zaidi ardhi.

"Mwaka 1994 hadi 2015 kulifanyika mabadiliko kutoka matumizi ya ardhi kwa kilimo kwenda makazi, uanzishwaji wa taasisi, ofisi ya Mthamini Mkuu wa Serikali, Ofisi ya Mrajis wa Ardhi na Bodi ya Kudhibiti Kodi za Nyumba," anasema huku akibainisha kuwa katika kipindi chote hicho baadhi ya sharia zilifutwa na zingine kubadilishwa.

**SEKTA YA MAKAZI**

Hadi mwaka 1964, Dk. Mngereza anasema nyumba chache zilikuwa zikimilikiwa na serikali na kuanzia wakati huo kumekuwa na mageuzi makubwa katika sekta hiyo. Anasema nyumba 4,461 zilijengwa zikiwamo 2,900 za ghorofa na nyumba za vijijini. Kwa upande wa Pemba, pia zilijengwa nyumba za ghorofa kama za Michenzani.

"Suala hili la makazi ni nyeti kutokana na ongezeko la idadi ya watu. Wakati wa Mapinduzi watu walikuwa chini ya 100,000 lakini sasa tuko zaidi ya milioni 1.8, hivyo tukaona tuwe na sheria kuhusu maendeleo ya makazi na ZHC ikapemwa jukumu wa kuendeleza suala hilo," anasema.

Kwa mujibu wa Katibu Mkuu, ulianzishwa mpango endelevu katika makazi kuhusu nyumba 723 za NHC na 685 za wananchi Michenzani kwa ajili ya utunzaji na jamii kushiriki katika usafi.

Aidha, anasema kutokana na nyumba nyingi kuwa katika hali mbaya, ukarabati mkubwa uli-

INAENDELEA UK. 16




# Maendeleo makubwa elimu miaka 60 Mapinduzi



Rais Dk. Hussein Ali Mwinyi akiwa na mke wake, Mama Maryam Mwinyi katika darasa la wanafunzi katika Shule ya Sekondari Tumekuja iliyopo Zanzibar

**INATOKA UK. 11**

Kutokana na ongezeko hilo, anasema serikali imeimarisha mikakati yake kupambana na ongezeko la watu na kuhakikisha hakuna Mzanzibari atakayekosa haki ya msingi ya kupata elimu popote alipo.

Khamis anasema yote hayo yanafanyika ili kuhakikisha wanafunzi wanasoma katika mazingira mazuri na kupata elimu bora kwa manufaa yao, jamii na taifa kwa ujumla.

"Serikali yetu inayoongozwa na Dk. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, inapambana kufikia shabaha ya wanafunzi wasiozidi 45 kwa darasa moja. Pia shule zote zinasomesha kwa mtindo wa shifti moja ya asubuhi pekee badala ya shifti mbili ya asubuhi na mchana," anasema.

Pia anasema inaimarisha miundombinu ya matumizi ya teknolojia na maabara za sayansi katika shule zote na hayo ndiyo malengo hasa ya Mapinduzi ya Zanzibar ya mwaka 1964.

Anasema serikali imejipanga kuendeleza jitahada za kuimarisha miundombinu kwa kutumia vyanzo vyake vya ndani lakini pia kwa kushirikiana na washirika wa maendeleo.

Anasema uwekezaji katika elimu utakwenda sambamba na upatikanaji wa vifaa mbalimbali vikiwamo vya kufundishia na kujifunzia, samani na walimu wenye sifa.

Katibu Mkuu anasema wakati serikali inatekeleza mikakati mbalimbali ya kuwaletea wananchi maendeleo, ni jukumu la kila mmoja kuhakikisha watoto wanaandikishwa shule na kuwasimamia ili kukamilisha elimu yao msingi na kuendelea na elimu ya sekondari.

Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali, Lela Mohamed Mussa, alimpongeza Rais Mwinyi kwa maendeleo anayoyaleta kwa wananchi wa Zanzibar ikiwamo sekta ya elimu. Anasema kwa hatua hiyo, aneonyesha kuyatendea haki Mapinduzi hasa katika kipindi yanapotimiza miaka 60.

Anasema uimarishaji wa elimu umeleta mafanikio makubwa kwa kuwa ni ufaulu wa wanafunzi hasa wa darasa la saba wanaopasi michepuo na vipawa kwa Desemba, 2023 umeongezeka kutoka wanafunzi 2,167 mwaka 2021 na mwaka 2023 ni wanafunzi 6,662.

Rais Mwinyi, anasema amefanya kazi kubwa katika sekta ya elimu na kuvuka lengo la Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2020 - 2025 ambayo imeelekeza kujengwa kwa shule 16 lakini shule zilizojengwa Unguja na Pemba ni 25.

> "Serikali yetu inayoongozwa na Dk. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, inapambana kufikia shabaha ya wanafunzi wasiozidi 45 kwa darasa moja. Pia shule zote zinasomesha kwa mtindo wa shifti moja ya asubuhi pekee badala ya shifti mbili ya asubuhi na mchana," anasema.

**KAULI YA MWINYI**

Rais Dk Mwinyi anasema Mapinduzi ya mwaka 1964 yamefungua fursa na huduma za maendeleo ya kijamii na kiuchumi Zanzibar, zikiwamo elimu,. Anasema serikali iliyoongozwa na Hayati Mzee Karume ilitangaza elimu bure kwa wananchi wote , hivyo ikawa haki ya msingi ya kila raia.

Dk. Mwinyi anasema SMZ inaendelea na mikakati ya kuifanyia sekta ya elimu mageuzi makubwa ili kuhakikisha ubora unaimarika na vijana wanapata elimu itakayowasaidia kumudu maisha pamoja na kupata wataalamu kwa maendeleo ya nchi.

Anasema mageuzi hayo yamezingatia kuimarisha miundombinu, uongozi na ufuatiliaji wa maendeleo ya elimu katika ngazi zote, kuanzisha tume ya walimu kwa ajili ya kusimamia masuala ya walimu, mitaala, kuimarisha vifaa vya kufundishia na kujifunzia na kuimarisha matumizi ya teknolojia.

Pia anasema lazima watoto kuandikishwa, kukamilisha elimu ya msingi na kuendelea na masomo katika ngazi zinazofuata na hatimaye kujiunga elimu ya vyuo vikuu ili nchi ipate wataalamu na kupiga hatua kubwa zaidi za maendeleo. Dk, Mwinyi anasema kufanya hivyo ni kuyaenzi Mapinduzi na kuitendea haki serikali ambayo imefanya juhudi kubwa kuhakikisha inaimarisha huduma za elimu.



# ZIPA mhimili ukuzaji wa uwekezaji Zanzibar

**Na Mwandishi Wetu**

UWEKEZAJI katika sekta yoyote ni mhimili mkubwa katika maendeleo ya kiuchumi na kijamii katika jamii na taifa lolote duniani. Uwekezaji huchochea ukuaji wa uchumi na kuongeza uzalishaji wa bidhaa kwa ajili ya mauzo ya ndani na nje, ajira kwa wananchi na ongezeko la mapato ya serikali kupitia kodi mbalimbali na mauzo ya bidhaa.

Katika kutambua hilo, Serikali ya Mapinduzi Zanzibar (SMZ) iliandaa mipango mbalimbali kwa ajili ya uwekezaji ili kuinua uchumi wa visiwa hivyo na maendeleo endelevu katika nyanya mbalimbali. Matokeo ya mipango hiyo yanaonekana sasa wakati Zanzibar inatimiza miaka 60 ya Mapinduzi.

"Pamoja na matokeo hayo, bila kuwa na sheria, miongozo, kanuni na taratibu huwezi kufanikisha haya. Kutokana na umuhimu wa uwekezaji, Zanzibar imepita katika hatua mbalimbali hadi sasa kuwa na Mamlaka ya Ukuzaji Uwekezaji Zanzibar (ZIPA).

"Lengo ni kuhakikisha kunakuwa na uwekezaji wenye mafanikio na kuleta maendeleo endelevu," anasema Mkurugenzi Msaidizi Uwezeshaji na Huduma wa ZIPA, Saleh Saad Ahmed alipohojiwa kuhusu hatua zilizofikiwa na Zanzibar katika kuchochea uwekezaji Zanzibar.



Mkurugenzi Mtendaji Mamlaka ya Kukuza Uwekezaji Zanzibar (ZIPA) Nd. Shariff Ali Sharif

Saleh anabainisha kuwa uwekezaji ndiyo mhimili mkuu katika maendeleo ya taifa lolote, Zanzibar ikiwamo. Anasema awali watalii wengi walikuwa wakienda Mombasa lakini baada ya vurugu zilizotokana na siasa katikati ya miaka ya 2000, hali ilibadilika na Zanzibar kuchukua nafasi.

"Mapinduzi yalikuja kuleta utawala bora na kuangalia nini hatima ya Zanzibar kiuchumi kwa miaka inayofuata. Viongozi waliotangulia kabla ya Rais Dk. Hussein Ali Mwinyi walianzisha mambo ambayo yameleta mafanikio makubwa kiuchumi Zanzibar. Rais Mwinyi ameendeleza zaidi na kuna matokeo makubwa katika ukuzaji uwekezaji na maendeleo kwa ujumla," anasema.

Mkurugenzi huyo anabainisha kwamba kutokana na kasi ya maendeleo ya utalii Zanzibar, uwekezaji umesaidia miradi mingi ya hoteli hivyo kuchangia kwa asilimia 25 hadi 30 ya pato zima la visiwa hivyo.

Kwa mujibu wa Saleh, kati ya miradi 1,255 iliyosajiliwa ZIPA, 600 ni ya hoteli kwa maana ya huduma za malazi na chakula na kwamba katika uongozi wa sasa wa Dk. Mwinyi kumekuwa na kasi kubwa katika usajili wa miradi ya uwekezaji.

"Tangu kikiwa kituo cha uwekezaji mpaka sasa ZIPA katika uongozi wa Dk. Mwinyi pekee, yaani miaka mitatu, kumekuwa na uwekezaji wa miradi ya Dola bilioni 12.4 za Marekani. Kabla ya hapo hakuna mwaka ambao iliwahi kusajiliwa Zaidi ya miradi 50.

"Katika kipindi cha Dk. Mwinyi, ilianza kusajiliwa miradi 99, ikafuata 96 na sasa tunakwenda miradi 104 hadi 105. Hiyo ni katika ZIPA peke yake, mingine inasajiliwa kwenye utalii na wazawa kwenye viwanda. Haya yote ni ni mafanikio makubwa ya Mapinduzi," anasema.

Anaongeza kuwa: "Kabla ya Mapinduzi hakukuwa na maendele kama haya au manufaa kwa wazawa. Lakini kwa sababu ya sheria na katiba zetu katika kuwajali wananchi, kumekuwa na mafanikio haya. Hata ongezeko la idadi ya watu linaonyesha kuwa Zanzibar panafaa kwa uwekezaji kwa sababu pana utulivu."

Kuhusu maendeleo kisekta, anasema uwekezaji mkubwa umefanyika katika miradi ya hoteli kwa

**INAENDELEA UK. 16**

SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR

**MAMLAKA YA UKUZAJI VITEGA UCHUMI ZANZIBAR (ZIPA)**

**MIAKA 60 YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR**



*Rais wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar*
*Mhe. Dr. Hussein Ali Mwinyi*






*Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania*
*Mhe. Dr. Samia Suluhu Hassan*

Bodi ya Wakurugenzi, Menejimenti na wafanyakazi wote wa Mamlaka ya Ukuzaji Vitega Uchumi Zanzibar (ZIPA) wanaungana na Mheshimiwa Mhe. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi na Mheshimiwa Dk Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika kuadhimisha miaka 60 ya Mapinduzi ya Zanzibar.

www.zipa.go.tz //////////////// #WEKEZA ZANZIBAR SASA!

# Utalii nguzo ya uchumi miaka 60 ya Mapinduzi

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR




SEKTA ya utalii ni mboni ya jicho la Uchumi wa visiwa vya Zanzibar na Tanzania kwa ujumla. Wakati Zanzibar ikiadhimisha miaka ya Mapinduzi, sekta hiyo inachangia uchumi wa visiwa hivyo kwa asilimia 29.2.

Katika kipindi hicho utalii pia umechangia kupatikana kwa ajira za mtu mmoja mmoja pamoja na vikundi vya wajasiriamali. Pia shughuli za utalii na mambo ya kale zimezidi kukua siku hadi siku na idadi ya wawekezaji imezidi kuongezeka katika maeneo ya kihistoria.

Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale, Simai Muhammed Said, anasema wizara hiyo inatekeleza majukumu ya kuitangaza Zanzibar kiutalii ndani na nje ya nchi. Anasema jukumu lingine ni kukuza pato la nchi kupitia sekta ya utalii, kuwashawishi wawekezaji wa ndani na nje ya nchi kuanzisha miradi mbalimbali ya utalii itakayotoa tija kwa wananchi, kuyalinda, kuyahifadhi na kuyatangaza maeneo ya kihistoria.

Serikali, anasema inaendelea kuvitunza vitu na mabaki ya kihistoria yaliyopo nchini ili kuweka kumbukumbu kwa faida ya kizazi cha sasa na kijacho, kuuhifadhi na kuuendeleza Mji Mkongwe wa Zanzibar ambao ni kivutio kikubwa cha watalii.

**MAFANIKIO**

Simai anasema wakati Zanzibar inaadhimisha miaka 60 ya Mapinduzi, sekta ya utalii imepata mafanikio mengi ikiwamo kuongezeka uwekezaji katika miradi ya utalii yaliyochagizwa na mageuzi ya kiuchumi katika miaka ya 1980.

Anasema serikali imeweka mazingira rafiki ya uwekezaji nchini kwa kutunga sera, sheria na kuweka miongozo mbalimbali.

Kutokana na juhudi hizo, Simai anasema uwekezaji katika utalii umeongezeka kutoka miradi 84 ya miaka ya 1990 hadi 1,544 mwaka 2021 na miradi hiyo inamilikiwa na wazawa, wageni au kwa ubia baina ya wazawa na wageni.

"Miradi hiyo imejumuisha hoteli, migahawa, waendesha utalii, kumbi za mikutano, maduka ya zawadi, michezo ya baharini na afya," anasema Simai na kubainisha kuwa baada ya Mapinduzi, Zanzibar kulikuwa na hoteli zisizozidi tano zikiwamo za Shangani, Bwawani na Amani ambazo zilitumiwa kama nyumba za kulala wageni.

Simai anasema ndani ya miaka 60 kuna zaidi ya hoteli 600 zenye hadhi kutoka nyota moja hadi tano.

> **"Kikosi hiki kimesaidia kwa kiasi kikubwa kupunguza matokeo ya uhalifu ndani ya sekta ya utalii na kuhakikisha wageni wanaotembelea Zanzibar wanakuwa salama pamoja na mali zao. Kikosi hiki kimezinduliwa rasmi Novemba, 2021 na Rais Dk. Hussein Ali Mwinyi," anasema Sima.**

**IDADI WATALII**

Kutokana na jitihada zinazofanywa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar za kuitangaza Zanzibar kiutalii ndani na nje ya nchi, Simai anasema kumekuwa na ongezeko kubwa la watalii wanaoingia. Anabainisha kuwa watalii hao ni kutoka 19,368 mwaka 1985 hadi kufikia watalii 548,503 mwaka 2022.

Simai anasema ongezeko hilo limechangiwa na jitihada za kutangaza utalii na kufunguliwa kwa jengo jipya la tatu la abiria (terminal III) katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Abeid Amani Karume, hivyo kuwa kichocheo kikubwa kwa mashirika ya ndege ya kimataifa kutua Zanzibar.

"Pamoja na hayo, bado mashirika mengine yameongeza safari za kutua nchini ambayo ni Ethiopia Airlines ambayo kwa sasa hutua kila siku, Oman Air, Fly Dubai, na Etihad. Ikiwa hali itaendelea vizuri, tunatarajia kufikia lengo la Ilani ya CCM ya wageni 850, 000 ifikapo mwaka 2025," anasema.

Simai anasema jitihada hizo zinakwenda sambamba na njia mpya za utandawazi wa matumizi ya teknolojia na kuzipa chapa huduma na bidhaa za utalii za Zanzibar na bidhaa hizo ni kama vile utamaduni, chakula, utalii wa mikutano, michezo na matamasha.

**JENGO LA ABIRIA**

Simai anasema ufunguzi wa jengo jipya la abiria katika Uwanja wa Ndege wa Karume umechangia kwa asilimia kubwa maendeleo ya sekta ya utalii hiyo ambapo mashirika mengi ya kimataifa yameanza kuleta wageni Zanzibar.

Anayataja mashirika hayo ni Royal Dutch Airlines (KLM), Edwelesis Airways, Air France, Etihad Airways, Hi Fly na Global Airways. Mashirika hayo yameweza kuiunganisha Zanzibar na nchi nyingi za Ulaya na Afrika.

Waziri Simai anasema wizara yake inaendelea kutangaza utalii bila ya kutumia gharama za fedha kwa kuwatumia mabalozi wa nchi ambao huchukua jitihada za hali ya juu za kuitangaza Zanzibar na kufanikisha kuja kwa wingi kwa wageni nchini.

"Wizara huwatumia waandishi wa habari wa kitaifa na kimataifa katika kuitangaza nchi. Tumekuwa tukishuhudia waandishi mbalimbali wa kimataifa wakiingia nchini na kuitangaza Zanzibar kwenye vyombo vyao vya kimataifa wanavyotoka," anasema.

**ONGEZEKO HOTELI**

Waziri Simai anasema kuwapo kwa hoteli za madaraja ya juu kumesaidia uimarishaji wa sekta ya utalii Zanzibar, hivyo kusababisha Zanzibar kutembelewa na wageni maarufu na wenye uwezo mkubwa kimatumizi.

Simai anasema ujenzi wa hoteli umeongezeka kutoka 620 mwaka 2020 hadi 709 kwa mwaka 2023 sawa na ongezeko la asilimia 15.

Pia kumekuwa na ongezeko la meli za utalii katika kukuza utalii nchini na wizara imekuwa ikiratibu na kupokea ujio wa meli hizo na kwa kipindi cha mwaka mmoja wizara imepokea meli saba za kitalii.

Alizitaja meli hizo kuwa ni Silver Shadow, Miss Artania, Le Jacques Cartier, MS Coral Geographer, MS Zuiderdam, MS Bolette na Swan Hellenic. Anasema meli hizo zimeleta watalii 3,774 na zimechangia katika kukuza pato la taifa na kuongeza idadi ya watalii.

**USALAMA WATALII**

Simai anasema ulinzi na usalama wa watalii na mali zao ni muhimu katika maendeleo ya sekta ya utalii. Katika kufanikisha azma hiyo, anasema serikali imeanzisha Kikosi cha Polisi Utalii na Diplomasia ambacho kina mchanganyiko wa askari kutoka vikosi vya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar na Polisi.

"Kikosi hiki kimesaidia kwa kiasi kikubwa kupunguza matokeo ya uhalifu ndani ya sekta ya utalii na kuhakikisha wageni wanaotembelea Zanzibar wanakuwa salama pamoja na mali zao. Kikosi hiki kimezinduliwa rasmi Novemba, 2021 na Rais Dk. Hussein Ali Mwinyi," anasema Sima.

Sambamba na hilo, anasema wizara imeratibu uchukuaji wa filamu ya The Royal Tour ambayo imewashirikisha Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Samia Suluhu Hassan na Dk. Mwinyi.

Anasema filamu hiyo imeitangaza Tanzania kimataifa kwa kuonyesha fursa zilizoko katika nyanja ya uwekezaji, utalii na uhusiano wa kimataifa.

Pia anasema kwa mara ya kwanza Kamisheni ya Utalii kwa kushirikiana na Jumuiya ya Umoja wa Mataifa inayoshughulikia Uchumi Afrika (UNECA) imeandaa mfumo wa upimaji wa mchango wa utalii kwenye pato la taifa.

Anasema kukamilika kwa mfumo huu kumewezesha kujulikana mchango halisi wa utalii katika pato la taifa na tayari ripoti hiyo imeshatolewa na imeshaanza kutumika.

**ONGEZEKO LA AJIRA**

Waziri Sima anasema sekta ya utalii inatoa mchango mkubwa katika kuwapatia vijana fursa za ajira nchini. Anasema kadri sekta inavyokua na nafasi za ajira nazo zinaongezeka na sasa inakisiwa ajira katika sekta ya utalii zimeongezeka kutoka ajira rasmi 12,000 na 30,000 zisizo rasmi katika miaka ya 2000 na kufikia ajira rasmi 33,000 na 100,000 zisizo rasmi mwaka 2022.

**ONGEZEKO MAPATO**

Kutokana na ongezeko la watalii na kukua kwa sekta ya utalii, kumekuwa na ongezeko la mapato. Anasema mapato hayo yanakwenda serikalini na mengine kwa wananchi wanaotoa huduma mbalimbali kwa watalii.

"Kwa mujibu wa Ripoti ya Utafiti wa Sekta ya Utalii Tanzania, Zanzibar ilipata Dola za Marekani milioni 844.9 mwaka 2022 ikilinganishwa na Dola milioni 71.3 mwaka 2004," anasema.

# Mageuzi sekta ya ardhi miaka 60 ya Mapinduzi

INATOKA UK. 12

hitajika kwa nyumba 4,161 Unguja na Pemba. Pia liliandaliwa andiko (proposal) ya kiufundi na kifedha na kuwasilishwa serikalini.

**MIPANGO MIKUBWA**

Ni dhahiri kwamba Zanzibar kumekuwa na ongezeko la watu huku ardhi ikibaki kuwa ile ile. Kutokana na ukweli huo, SMZ iliandaa mipango a muda mfupi, wa kati na muda mrefu kwa ajili ta kupata suluhisho la changamoto hiyo.

Katibu Mkuu anabainisha kuwa katika kufanya hivyo, serikali imedhamiria kuimarisha uongozi wa sekta ya ardhi na kwamba kuna kampuni ya Ufaransa ambayo iliandaa andilo mradi (feasibility study) na kupendekeza masuala ya ardhi, ikiwamo upimaji na mipango miji yanawekwa katika mfumo wa kiditali.

"Suala hilo limeshafanyika na kluwasilisha kwa serikali. Tunatarajia kuwa ndani ya januarii, mwaka huu tutaanza utekelezaji. Kwa hiyo masuala ya usajili wa ardhi yatakuwa katika mfumo wa kidogotali na itafanyika kwenye ngfazio za mikoa.

Hii ilishafanyika awali lakini kasi yake ilikuwa ndogo. Lakini tumeamua Kwenda kwa kasi zaidi kama Mheshimiwa Rais anavyotaka hasa kutokana na kasi ya uwekezaji, hivyo tunatamani watu wapimiwe na kupata ardhi ndani ya muda mfupi usiozidi wiki mbili," anasema.

Mpango mwingine, kwa mujibu wa Katibu Mkuu, ni kuanzisha kituo cha umahiri cha masuala ya uopimaji wa ardhi (National Geoinformation Cente) kwa ajili ya kuwafundisha wataalamu wa ardhi ambao watakuwa na uwezo wa kutoa huduma za viwango na kwa kasi. Changamoto nyingine iliyokuwapo awali ni uchelewaji wa vibali vya ujenzi. Anasema upatikanaji wa vibali ulikuwa unachukua muda mrefu, hivyo wamechukua hatua hizo za kuingia katika mfumo wa kidijitali na kufanya ugatuzi hadi ngazi ya halmashauri.

Kuhusu mipango miji, anasema serikali inalisimamia kikamilifu ili kuhakikisha kila kitu kinafanyika kwa mujibu wa upangaji wa matumizi ya ardhi kama vile ujenzi wa nyumba na maeneo ya huduma.

Moja ya mambo yanayotiliwa mkazo, anasema ni udhibiti wa ujenzi holela wa makazi na vituo vya mafuta. Anasema sheria ilianzishwa kuhusu udhibiti huo na kwamba wale waliobainika kujenga baada ya sheria hiyo, walivunjiwa.

"Lengo ni kuhakikisha kila kipande cha ardhi kinakuwa katika mpango maalum wa matumizi ya ardhi. Suala la ujenzi wa vituo vya mafuta liko chini ya ZURA (Mamlaka ya Udhibiti wa Nishati na Maji Zanzibar) kwahiyo mtu hawezi kuingia tuna jenga kituo bila kibali.

**NYUMBA ZA NAFUU**

Moja ya malengo makuu ya Mapinduzi ambayo yametimiza miaka 60 yalikuwa ardhi na makazi na moja ya mambo ya kuzingatia katika hilo ni kuwa na nyumba au makazi ya bei nafuu kwa wananchi wa kipato cha chini.

"Nyumba za bei nafuu si kwa wote lakini kama alivyoagiza Rais, jambo hili linatekelezwa. Makandarasi sita wameshapatikana kwa ajili ya utekelezaji na wameleta mapendelezo ya kifedha na kiufundi. Maeneo 22 yametengwa Unguja na Pemba na ujenzi wa nyumba 1,000 unatajiwa kuanza na kila wilaya tunapeleka mradi huo," anasema.

Pamoja na mpango huo, anakiri kwamba ZHC tangu kuanzishwa haijawahi kutekeleza mradi ya nyumjba za bei nafuu na ilipata changamoto katika kuhudumia nyumba zilizokuwapo. Lakini, anasema serikali imekuwa imara na baadhi ya watu waliokuwa wakikaa katika nyumba hizo wameanza kulipia.

Hata hivyo, Dk. Mngereza anasema shirika limeshaanzisha miradi ya ujenzi wa nyumba 72 katika eneo la Kwa Mchina na hadi Oktoba, mwaka jana, ilishauza asilimia 80 ya nyumba hizo.

"Rais alitoa Sh. Bilioni sita kat ya Sh. Bilioni 9.8 za mradi wa nyumba za bei nafuu za vyumba viwili hadi vitatu kwa ajili ya kuwauzia wananchi. Kwa kweli kumekuwa na meitikio mkubwa . Kuna mredi wa nyumba 150 Kisakasak na njia ya Fumba," anasema.

Ili kufanikisha mpango huo, Katibu Mkuu anasema wameshirikisha sekta binafsi kwa kuwaalika wawekezaji na kwamba walikutana nao June na Agosti, mwaka jana, wakaeleza changamoto wanazokabiliana nazo zikiwamo sheria.



# Takwimu zinavyoleta taswira halisi ya maendeleo ya kiuchumi, kijamii

**Na Mwandishi Wetu**

TAKWIMU ni suala muhimu kwa ajili ya mipango ya maendeleo ya kiuchumi na kijamii kuanzia ngazi ya chini hadi ya juu, kwa maana ya serikali. Bila kuwapo kwa takwimu sahihi, ni vigumu kupanga mipango pamoja na mgawanyo wa rasilimali katika jamii husika.

Hiyo inajidhihirisha kwa Zanzibar kuhusu umuhimu wa takwimu katika kuleta maendeleo endelevu katika sekta mbalimbali za kiuchumi na kijamii. Suala la takwimu kwa Zanzibar lilianza kabla ya Mapinduzi na limeendelea ndani ya miaka 60 ya Mapinduzi ya Zanzibar ya mwaka 1964 yaliyoleta ukombozi kwa wananchi.

Kabla ya Mapinduzi, kuanzia miaka ya 1930, takwimu kwa upande wa Zanzibar zilikuwa zinachukuliwa na Sensa ya Watu na Makazi iliyofanyika mwaka 1932 wakati huo idadi ya watu ilikuwa takribani 180,000.

Takwimu ziliendelea mpaka mwanzoni mwa miaka ya 1950 na sensa ya watu ilifanyika mwaka 1958 chini ya Afrika Mashariki ambayo ilibainisha kuwa idadi ya watu ilikadiriwa kuwa 285,000.

Zanzibar ilipofanya Mapinduzi Januari 12 mwaka 1964, shughuli za Takwimu na Sensa ya Idadi ya Watu zilihamishiwa kwenye seksheni ya Wizara ya Fedha. Mwaka 1967 Sensa ya Watu na Makazi ambayo ilikuwa ni ya Jamhuri, ilifanyika na idadi ya watu ilifika takribani 360,000. Sensa ya pili baada ya Mapinduzi, ilifanyika mwaka 1978. Takwimu ziliendelea kukusanywa ili kuimarisha uchumi na kupanga maendeleo kupitia Ofisi ya Kudumu ya Mipango (OKM) ambayo ilikuwa chini ya Wizara ya Fedha.

Mwaka 1979, Rais wa Awamu ya Pili Zanzibar, Aboud Jumbe Mwinyi, alitoa tamko la kuanzishwa kwa Idara ya Takwimu Zanzibar. Idara hii ilikusanya takwimu za kiuchumi na kijamii kwa ajili ya maendeleo ya nchi.

Sensa ya tatu baada ya Mapinduzi ilifanyika mwaka 1988 kwa kuangalia Idadi ya Watu na Makazi na kwa mujibu wa Mtakwimu Mkuu wa Serikali, sensa ile ilifanyika kwa mafanikio makubwa na ofisi iliendelea kufanya kazi zake.

Mnamo mwaka 2002, Tanzania ilifanya sensa ya nne na kubainika kuwa Zanzibar ilikuwa na watu 981,754. Sensa ya tano ilifanyika mwaka 2012 ikafahamika kuwa Zanzibar ina jumla ya watu wanaokadiriwa kufikia 1,303,055

Sensa ya sita ni ya mwaka 2022 ambapo imebainisha kuwa Zanzibar ina watu 1,887,724.

"Mafanikio ya sensa hii ni makubwa sana. Kwanza mwitikio wa wadau ulikuwa mkubwa na haukuwa na changamoto yoyote. Matokeo yalikuwa na kiu kubwa ya kutumia taarifa hizi.

"Taarifa za sensa hii zilitolewa mapema kutokana na mifumo ya kidijitali iliyotumika.

Waandishi wa habari pia walitoa wito mkubwa kwa wananchi ili kushiriki katika sensa ya watu na makazi," anasema Salum Kassim Ali, Mtakwimu Mkuu wa Serikali Zanzibar.

**HISTORIA**

Kuanzia mwaka 1990 ofisi iliendeleza kasi ya ukusanyaji wa takwimu Mwaka 1999 ofisi ya Mtakwimu ilitunga sheria mpya ya Ofisi ya Mtakwimu Zanzibar. Ilipofika mwaka 2007, ilitungwa sheria nyingine na kuitwa Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali na Iliongeza Bodi ya Takwimu Zanzibar ambayo mpaka sasa ipo na inasimamia ofisi hii.

Mwaka 1968 zilijengwa nyumba za Mjerumani, nyumba za Kilimani, Michenzani, Bambi Makunduchi na kwa upande wa Pemba zilijengwa Wete , Chakechake na Mkoani.

**UMUHIMU WA TAKWIMU**

Idadi ya watu ndiyo inayotumika wakati wa uandikishaji wa wapiga kura. Uchaguzi wa mwaka 1957 na 1961 na 1963. Ulitumia sensa ya watu na makazi.

Umuhimu mwingine ni kupanga mipango ya kiuchumi na maendeleo ya nchi kama barabara na miundombinu ,uendelezaji wa majumba ya makazi na umuhimu mwingine ni ukusanyaji wa Takwimu, uchakataji pamoja na usambazaji wa Takwimu.

**MAFANIKIO**

Mafanikio ya takwimu, kwanza, ni ukusanyaji wa taarifa na upashaji taarifa mbalimbali kwa serikali na pili, ni utolewaji wa matoleo mbalimbali ya kiuchumi, mfumo wa bei , ajali na ripoti mbalimbali. Umuhimu mwingine ni utafiti mwingi umefanywa kupitia ofisi ya Mtakwimu.

Upande wa watendaji, miaka ya 1970 mpaka 1990 watendaji wachache walikuwa na uwezo lakini sasa hivi vijana wengi wana elimu. Wafanyakazi wasiopungua 30 wana shahada ya kwanza na 25 shahada ya pili na wengi ni wa diploma na cheti.

Aidha, mipango ya serikali kupitia Baraza la Wawakilishi imekuwa ikipangwa kupitia Takwimu hizi.

Mafanikio mengine ni ujenzi wa jengo la Pemba kwani tayari wameshafunga mkataba na kampuni ya kuandaa michoro ya jengo la Pemba. Ndani ya mwaka mmoja na nusu, jengo la Pemba litakuwa limekamilika. Kwa upande wa miundombinu ya ofisi, jengo ni zuri sana.

Kuna uhusiano mzuri sana na Ofisi ya Taifa ya Takwimu, Ofisi za Takwimu za Afrika Mashariki na za Dunia. Pia washirika wa Maendeleo kama UNICEF, UNDP na Benki Dunia.

**WITO KWA WANANCHI**

Takwimu ndiyo msingi wa kupanga na utakapopanga vizuri kupitia takwimu, maendeleo yatakwenda vizuri.

SERIKALI YA MAPINDUZI ZANZIBAR
OFISI YA MTAKWIMU MKUU WA SERIKALI

Maadhimisho
ya Miaka
ya Mapinduzi



1964 - 2024



BODI,MENEJIMENT NA WAFANYAKAZI WA OFISI YA MTAKWIMU MKUU WA SERIKALI ZANZIBAR, WANAMPONGEZA DKT HUSSEIN ALI MWINYI RAIS WA ZANZIBAR NA MWENYEKITI WA BARAZA LA MAPINDUZI PAMOJA NA WANANCHI WOTE WA ZANZIBAR KATIKA KUADHIMISHA MIAKA 60 YA MAPINDUZI MATUKUFU YA MWAKA 1964

TAKWIMU KWA MAENDELEO

Mh. Dr.Hussein Ali Mwinyi
Rais wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar

MUNGU IBARIKI ZANZIBAR
# TAKWIMU KWA MAENDELEO!

# ZIPA mhimili ukuzaji uwekezaji Zanzibar

**Inatoka uk. 14**

sababu ya ongezeko la watalii. Kwa sasa anasema kuna wastani wa watalii 600,000 wanaoingiza Zanzibar kwa mwaka na hoteli zilizoko ni 400.

Sababu kubwa ya ongezeko hilo, anasema ni sera na mikakati bora ya serikali katika kukuza uwekezaji katika sekta mbalimbali, utalii ukiwamo. Anasema sera hizo na sheria zimesababisha kutokuwapo kwa udhalilishaji dhidi ya wageni na wazawa na vitendo kama hivyo vikiripotiwa na kubainika ni kweli, mtu anachukuliwa hatua mara moja na kama ni mtalii au mgeni, anaondolewa mara moja.

**SEKTA YA MILKI**

Kutokana na wimbi la uwekezaji kuwa kubwa Zanzibar, Saleh anasema kumekuwa na kasi katika maendeleo ya sekta ya makazi hivi sasa. Kwa mujibu wa mkurugenzi huyo, hivi sasa kuna miradi 114 ya uwekezaji katika sekta hiyo imeandikishwa jambo linalodhihirisha kuwa kuna umuhimu wa kuwekeza katika eneo hilo.

Anasema katika kuwavutia wawekezaji wa sekta hiyo, mtu anayeuza nyumba yenye thamani ya Dola za 100,000 za Marekani anapata hati ya ukaazi. Pia watu wanashajihishwa kutokufunga nyumba wanapoondoka bali wakodishe ili kodi za serikali ziendele kulipwa.

"Katika hili lengo tunataka kuifanya Zanzibar kuwa sehemu ya pili ya ukaazi kwa watu (second home) kama ilivyo Dubai. Mtu ana nyumba Dubai na sehemu nyingine, ndivyo tunavyotaka Zanzibar iwe," anasisitiza.

Ili kuhakikisha wawekezaji hawapati usumbufu katika kupata vibali na vyeti kwa ajili ya kuanzisha miradi Zanzibar, Saleh anasema kwa mara ya kwanza masuala ya uwekezaji yameanza kufanyika kwa njia ua mtandao.

"Kupitia mfumo huu wa kielektroniki anapata cheti kupitia mtandaoni na malipo anafanya kwa njia ya mtandao. Tayari maombi 90 yamefanyika na wawekezaji wamepata vyeti kwa njia ya mtandao. Mfumo huu pia unaokoa muda ma fedha.

"Kupitia mfumo huu wa Zanzibar Investment Electronic Window, masuala yote yamefungamanishwa pamoja yakiwamo uhamiaji, ardhi. Katika kutoa huduma bora, kimeanzishwa kituo cha huduma kwa pamoja ambacvho kinahusisha uhamiaji, Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Mamlaka ya Mapato Zanzibar (ZRA), wakala wa Majengo (ZBA), utalii, manzigira na watu wa ardhi," anasema.



**MAGEUZI MAKUBWA**

Tangu ilipokuwa Idara ya Uwekezaji chini ya Wizara ya Fedha na Uchumi mwaka 1986 hadi mamlaka sasa, kumekuwa na mageuzi makubwa katika masuala ya uwekezaji Zanzibar.

Moja ya mafanikio ni kumtambua Mzanzibari na Mtanzania aliyeko ughaibuni (diaspora) tofauti na awali alivyokuwa akionekana mgeni. Pia mabadiliko ya sheria kuhusu uwekezaji yanawataka wawekezaji kurejesha kwa wananchi sehemu ya faida wanayopata (CSR).

Mafanikio mengine ni kuwawezesha wawekezaji kupata ardhi kwa ajili ya kuweeza miradi yao pamoja na kupunguza viwango wanavyopaswa kulipa. Viwango hivyo, kwa mujibu wa Saleh, kwa Watanzania vimepungua kutoka Dola 300,000 za Kimarekeni hadi Dola 200,000 na kwa wageni kutoka Dola milioni 2.5 hado Dola 500,000.

Ili kufanikisha azma ya uwekezaji, ZIPA imetenga maeneo huru sehemu mbalimbali ambayo hutulewa kwa wawekezaji. Baadhi ya maeneo hayo ni Free Economic Zone Fumba (hekta 3,000), Viwanda Vidogo Amani (hekta 12.6), Bandari Huru Maruhubi (hekta 5.6), Micheweni (hekta 808.8), mashamba ya mipira na visiwa kwa ajili ya uwekezaji.

**MIPANGO 2024**

Katika mwaka 2024, ZIPA imepanga kupita mkoa kwa mkoa na vyuo kutoa elimu kuhusu uwekezaji ikiwamo kuwamo kwa kampuni za ndani za ushauri elekezi katika masuala hayo. Pia imepanga kusimamia uwajibikaji wa wawekezaji kutekeleza utoaji wa misaada ya maendeleo ya jamii zilizoko katika maeneo ya uwekezaji (CSR) kulingana na mipango ya mikoa.

"Pia tunataka wananchi watangaze dhamira zao katika uwekezaji. Wengi wanakosa mitaji kwa maana ya fedha na uelewa wa masuala ya uwekezaji. Lengo hapa ni kuhakikisha mwananchi wa kawaida anajumuishwa na kusaidiwa katika masuala ya uwekezaji," anasisitiza Saleh.

SERIKALI YA MAPINDUZI ZANZIBAR
WIZARA YA UTALII NA MAMBO YA KALE- ZANZIBAR

MAADHIMISHO
ya Miaka
ya Mapinduzi



1964 - 2024

BODI,MENEJIMENT NA WAFANYAKAZI WA WAZIRI WA UTALII NA MAMBO YA KALE - ZANZIBAR, WANAMPONGEZA DKT HUSSEIN ALI MWINYI RAIS WA ZANZIBAR NA MWENYEKITI WA BARAZA LA MAPINDUZI PAMOJA NA WANANCHI WOTE WA ZANZIBAR KATIKA KUADHIMISHA MIAKA 60 YA MAPINDUZI MATUKUFU YA MWAKA 1964



Mh. Dr.Hussein Ali Mwinyi
Rais wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar

MUNGU IBARIKI ZANZIBAR

# ZAWA YAMALIZA KERO YA UPATIKANAJI WA MAJI SAFI

**Na Mwandishi Wetu**

Wakati Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ikiazimisha miaka 60 ya Mapinduzi Mamlaka ya Maji Zanzibar (ZAWA) Mamlaka pekee ya kushughulikia maji imeweza kuwapatia wananchi maji safi na salama.

Hii ni kutokana na mikakati iliyowekwa na mamlaka hiyo kupitia uwezeshwaji wa serikali ya awamu ya nane inayoongozwa na Dk. Hussein Ali Mwinyi.

Mkurugenzi Mkuu wa ZAWA , Mhandisi Dk. Salha Mohamed Kassim anasema, "anamshukuru sana Rais wa awamu ya nane kwa kuwapa kipaumbele sekta ya maji kwa kutekeleza miradi miwili mikubwa sana uzalishaji wa miradi hii unaweza kushinda zile awamu saba zilizopita.

Pia ameongeza kuwa, kazi kubwa ya mamlaka hiyo ni kuchimba visima , kazi nyingine ya mamlaka ni kuyasafisha maji hayo na kuyahifadhi kwenye visima. Pamoja na kuyahifandi kwenye matanki makubwa.na kuyafikisha kwa wananchi.

Kwa sasa kuna utekelezaji wa miradi miwili mikubwa ya maji ,mradi mmoja ni mkopo wa exim Bank kupitia serikali ya India. Ambao ni wa Dola milioni 92.18. kupitia mradi huo zawa imeweza kuchimba visima vikubwa 64. Visima hivi vina uwezo wa kuzalisha maji lita milioni 177 kwa siku. Kabla ya miradi hii zawa ilikuwa na uwezo wa kuzalisha maji lita milioni 143. Kutoka kwenye visima vidogo na vya wastani 308.

Zawa iliweka mkakati wa kuwa na kisima zaidi ya kimoja na kujaza maji kwenye tanki moja. Ili kuondoa kero ya ukosefu wa maji kwa wananchi. Zawa imetengeneza mifumo saba ya maji. Ya kwanza ipo Dole, ya pili ipo Mfenesini, ya tatu ipo dimani ya nne ipo Mkoroho, ya tano Maungani, ya sita Masingini na ya saba ipo Kwarara,. Kupitia mifumo yote saba kuna jumla ya matanki 15 yenye uwezo wa kuhifadhi maji lita milioni 134 matanki yote yakijaa. Ambayo yanatoka kupitia visima 64, haya ni mafanikio makubwa sana ambayo hayajawahi kutokea awamu zote za nyuma. Matanki haya kumi na tano. Mawili yapo Mfenesini, mawili yapo Dole, Kwarara kuna matanki matatu. Kubwa la chini lina uwezo wa kuhifadhi lita milioni 32.5 juu zipo mbili kila moja lina uwezo wa kuhifadhi maji lita milioni 5.5.Kwarara peke yake ina uwezo wa kuhifadhi maji lita milioni 43.5 .

Matanki yote 15 ambayo Kwarara 3 , Mfenesini 2,Dole 2, Dimani 2, Mkorogo 2, pamoja na Masingini 2. Zawa imelaza mabomba ya km 480 kutoka kwenye visima. Kuleta kwenye matanki na kutoka kwenye matanki na kupeleka kwa wananchi.

Dk. Salha anasema,mradi huu utakwenda kuwapatia maji shehia 36 za mkoa wa mjini magharibi pamoja na vitongoji vya karibu yake. Wananchi wote watafungiwa mita za maji.

Awali zilizopita walifunga mita zisizofikia 20,000 sasa hivi mamlaka hiyo ina uwezo wa kupima mwananchi anatumia maji kwa kiasi gani na atalipia kiasi gani. Ili mwananchi aweze kutumia maji kwa uangalifu na kuweza kutoa huduma zinapotokea hitilafu za maji. Haya ni mafanikio ambayo yamepatikana katika miaka 60 ya mapinduzi.

Mafanikio mengine ni ujenzi wa ofisi bora na ya kisasa iliyopo Madema 27.12.2023

Mafanikio mengine ni ununuzi wa magari kwa wahandisi. Kuna wakandarasi 3. Megha, Hellen T na Afcon. Magari haya yanawasaidia wahandisi ili kusimamia kazi. Pamoja na kununua mita za kufunga kwenye shehia 36.

Mradi wa ahueni ya uviko 19

Vilevile mradi wa ahueni uviko 19 ni wa Sh. 34.2bilioni. Zawa itafungua miradi midogo 10.

Kwenye mradi wa exim Zawa watafungua miradi 4. Jengo na miradi mitatu . Moja Dimani nyingine Masingini na Dole. Wananchi washaanza kupata maji katika sehemu hizo tatu.

Pesa hizi ziliweza kuongeza visima vipya 38 ambapo walijenga matanki 10. 5 yapo Pemba na 5 yapo Unguja. Kila tanki lina ujazo wa lita milioni moja. Zawa imeongeza uhifadhi wa maji wa lita milioni 10. Ukiunganisha na matanki ya exim Zawa imeweza kuhifadhi maji lita milioni 144.

Zawa pia imetengeneza visima 36. Kwa kuweka miundombinu na kubadilisha pampu kwenye visima vya zamani 49 na kununua pampu 123 na kuimarisha huduma ya maji safi na salama na pampu 64 kwenye mradi wa exim Bank. Zawa imemaliza tatizo la maji katika kisiwa cha Tumbatu kwa kuwawekea tanki la maji lenye ujazo wa lita milioni moja.

Matanki 2 yapo mkoa wa kaskazini Pemba makangale na shumba na shanjani mkoa wa kusini.

Matanki ya Unguja yapo Bubwini na katika kisiwa cha Tumbatu. Pamoja na bambi ukuja ukuu na Mgeni Haji.

Pia Zawa imejenga vibanda 52 vya kuhifadhia pampu hizo. Vibanda 26 vipo Pemba na vibanda 26 vipo Unguja. Na visima 38 27 vilichimbwa Pemba na 11 vimechimbwa Unguja. Na Zawa imenunua magari 2 ya kuchimbia visima.

Pia zawa imetumia sehemu ya fedha hizo kulaza mabomba km 319. Hatua hii bado haijakamilika. Km 200 tayari kwa Unguja na Pemba. Zawa pia imenunua mashine za kuunganishia mabomba 13 na majenereta 10 ili kufanya kazi kwa haraka.

Mradi mpya

Zawa inao mradi mpya wa KFW ambao utaanza hivi karibuni. Na mradi wa JAICA ambao nao karibu utaanza. Na mradi wa mwekezaji NEC "National energy sector " ya Oman. Pia zawa wametia saini MOU ya Mradi wa SCAN INVESTMENT kwa ajili ya kuweka solar kwenye visima.

Mfumo

Pia Zawa inatumia mifumo mbalimbali ya kielektroniki. Pamoja na Tehama kuhakikisha inafikisha bili kwa wananchi , pamoja na kupokea pesa kupitia kwenye mfumo. Unaweza kutumia simu yako ya mkononi kulipia maji. Au wakala wa bamk tofauti kama PBZ, CRDB,NMB na benki nyingine. Zawa inatumia pia smart mita pia watafunga mita zaidi ya 20,000.

Malengo makubwa ya Zawa ni kuhakikisha Wananchi wanapata maji kwa asilimia 100. Baada ya kufungua miradi yote.







# ZAWA yamaliza kero ya upatikanaji wa Maji Safi na Salama Zanzibar



***Na Mwandishi wetu***

Wakati Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ikiazimisha miaka 60 ya Mapinduzi Mamlaka ya Maji Zanzibar (ZAWA) Mamlaka pekee ya kushughulikia maji.imeweza kuwapatia wananchi maji safi na salama.

Hii ni kutokana na mikakati iliyowekwa na mamlaka hiyo kupitia uwezeshwaji wa serikali ya awamu ya nane inayoongozwa na Dkt. Hussein Ali Mwinyi.

Mkurugenzi Mkuu wa ZAWA , Mhandisi Dkt. Salha Mohamed Kassim anasema, "anamshukuru sana Raisi wa awamu ya nane kwa kuwapa kipaumbele sekta ya maji kwa kutekeleza miradi miwili mikubwa sana . uzalishaji wa miradi hii unaweza kushinda zile awamu saba zilizopita.

Pia ameongeza kuwa, Kazi kubwa ya mamlaka hiyo ni kuchimba visima . kazi nyingine ya mamlaka ni kuyasafisha maji hayo na kuyahifadhi kwenye visima. Pamoja na kuyahifandi kwenye matanki makubwa.na kuyafikisha kwa wananchi.

Kwa sasa kuna utekelezaji wa miradi miwili mikubwa ya maji . mradi mmoja ni mkopo wa exim Bank kupitia serikali ya India. Ambao ni wa Dola milioni 92.18. kupitia mradi huo zawa imeweza kuchimba visima vikubwa 64. Visima hivi vina uwezo wa kuzalisha maji lita milioni 177 kwa siku. Kabla ya miradi hii zawa ilikuwa na uwezo wa kuzalisha maji lita milioni 143. Kutoka kwenye visima vidogo na vya wastani 308.

Zawa iliweka mkakati wa kuwa na kisima Zaidi ya kimoja na kujaza maji kwenye tanki moja. Ili kuondoa kero ya ukosefu wa maji kwa wananchi. Zawa imetengeneza mifumo saba ya maji. Ya kwanza ipo Dole, ya pili ipo Mfenesini, ya tatu ipo dimani ya nne ipo mkoroho, ya tano Maungani, ya sita Masingini na ya saba ipo kwarara,. Kupitia mifumo yote saba kuna jumla ya matanki 15. yenye uwezo wa kuhifadhi maji lita milioni 134 matank yote yakijaa. Ambayo yanatoka kupitia visima 64, haya ni mafanikio makubwa sana ambayo hayajawahi kutokea awamu zote za nyuma. Matanki haya kumi na tano. Mawili yapo mfenesini, mawili yapo dole, kwarara una matanki matatu. Kubwa la chini lina uwezo wa kuhifadhi lita milioni 32.5 juu zipo mbili kila moja lina uwezo wa kuhifadhi maji lita milioni 5.5.kwarara peke yake ina uwezo wa kuhifadhi maji 43.5 milioni lita,

Matanki yote 15 ambayo kwarara 3 , mfenesini 2,dole 2, dimani 2mkorogo 2, pamoja na masingini 2.moja chini na moja juu ya mnara.

Zawa imelaza mabomba ya km 480 kutoka kwenye visima. Kuleta kwenye matanki na kutoka kwenye matanki na kupeleka kwa wananchi.

Dkt Salha anasema,mradi huu utakwenda kuwapatia maji shehia 36 za mkoa wa mjini magharibi pamoja na vitongoji vya karibu yake. Wananchi wote watafungiwa mita za maji.

Awali zilizopita walifunga mita zisizofikia 20,000 sasa hivi mamlaka hy ina uwezo wa kupima mwananchi anatumia maji kwa kiasi gani na atalipia kiasi gani. Ili mwananchi aweze kutumia maji kwa uangalifu. Na kuweza kutoa huduma zinapotikea itilafu za maji. Haya ni mafanikio ambayo yamepatikana katika miaka 60 ya mapinduzi.

**Mafanikio mengine ni ujenzi wa ofisi bora na ya kisasa. Iliyopo madema 27.12.2023**

Mafanikio mengine ni ununuzi wa magari kwa wahandisi. Kuna wakandarasi 3. Megha, Hellen T na Afcon. Magari haya yanawasaidia wahandisi ili kusimamia kazi. Pamoja na kununua mita za kufunga kwenye shehia 36.

**Mradi wa ahueni ya uviko 19**



Vilevile mradi wa ahueni uviko 19 ni wa sh. 34.2bilioni. zawa itafungua miradi midogo 10. Miradi mitatu ni ya exim bank. Na 6 ya ahueni covid 19 na 1 ni wa jengo la mamlaka hiyo.

Kwenye mradi wa exim zawa watafungua miradi 4. Jengo na miradi mitatu . Moja dimani nyingine masingini na dole. Wananchi washaanza kupata maji katika sehemu hizo tatu.

Pesa hizi ziliweza kuongeza visima vipya 38 .ambapo walijenga matanki 10. 5 yapo pembe na 5 yapo unguja. Kila tanki lina ujazo wa lita milioni moja. Zawa imeongeza huifadhi wa maji wa lita milioni 10. Ukiunganisha na matanki ya exim zawa imeweza kuhifadhi maji lita milioni 144.

Zawa pia imetengeneza visima 36. Kwa kuweka miundombinu. Na kubadilisha pampu kwenye visima vya zamani 49 na kununua pampu 123 na kuimarisha huduma ya maji safi na salama.na pampu 64 kwenye mradi wa exim Bank. Zawa imemaliza tatizo la maji katika kisiwa cha Tumbatu kwa kuwawekea tanki la maji lenye ujazo wa lita milioni moja.

Matanki 2 yapo mkoa wa kaskazini pemba makangale na shumba na shanjani mkoa wa kusini. Jingine kujini na kendwa pemba.

Matanki ya unguja yapo bubwini na katika kisiwa cha Tumbatu. Pamoja na bambi ukuja ukuu na Mgeni Haji.

Pia zawa imejenga vibanda 52 vya kuhifadhia pampu hizo. Vibanda 26 vipo pemba na vibanda 26 vipo unguja. Na visima 38 27 vilichimbwa pemba na 11 vimechimbwa unguja. Na zawa imenunua magari 2 ya kuchimbia visima.

Pia zawa imetumia sehemu ya fedha hizo kulaza mabomba km 319. Hatua hii bado haijakamilika. Km 200 tayari kwa unguja na Pemba. Zawa pia imenunua mashine za kuunganishia mabomba 13 na majenereta 10 ili kufanya kazi kwa haraka.

**Mradi mpya**

Zawa inayomradi mpya wa KFW ambao utaanza hivi karibuni. Na mradi wa JAICA ambao nao karibu utaanza. Na mradi wa mwekezaji NEC "National energy sector " ya Oman. Pia zawa wametia saini MOU ya Mradi wa SCAN INVESTMENT kwaajili ya kuweka solar kwenye visima.

**Mfumo**

Pia Zawa s inatumia mifumo mbalimbali ya kielectronic. Pamoja na Tehama kuhakikisha inafikisha bill kwa wananchi , pamoja na kupokea pesa kupitia kwenye mfumo. Unaweza kutumia simu yako ya mkononi kulipia maji. Au wakala wa bamk tofauti kama PBZ, CRDB,NMB na benki nyingine. Zawa inatumia pia smart mita pia watafunga mita Zaidi ya 20,000.

Malengo Makubwa ya Zawa ni kuhakikisha Wananchi wanapata maji kwa asilimia 100. Baada ya kufungua miradi yote.

MAMLAKA YA MAJI ZANZIBAR

ZAWA
Zanzibar Water Authority

MIAKA 60 YA
MAPINDUZI YA ZANZIBAR
1964 - 2024

Bodi ya wakurugenzi ,Uongozi na Wafanyakazi wote wa Mamlaka ya Maji Zanzibar (ZAWA)wanatoa pongezi kwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Zanzibar Dkt. HUSSEIN ALI MWINYI katika kuadhimisha miaka 60 ya Mapinduzi.
Mamlaka ya Maji Zanzibar tunaahidi kuendelea kuyalinda Mapinduzi yetu kwa kutoa huduma bora za Maji Safi na Salama kwa Wazanzibar wote.

" KILA TONE NI GHARAMA TUMIA MAJI KWA UANGALIFU"

FACEBOOK INSTA TWITTER Mamlaka ya Maji Zanzibar-ZAWA



Mh. Dr.Hussein Mwinyi
Rais wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar

Kwa Maelezo zaidi
Tupigie: +255 24 223 1151, Email: info@zawa.go.tz, www.zawa.go.tz

## ZISIKUPITE

### HAALAND NAYE MADRID

KLABU ya Real Madrid inatathmini uwezekano wa kumsajili mshambuliaji wa Manchester City na Norway, Erling Haaland mwenye umri wa miaka 23, kwa sababu ya wasiwasi iwapo fowadi wa Ufaransa, Kylian Mbappe mwenye umri wa miaka 25, ataondoka Paris St-Germain ili kujiunga nao. **(AS)**

### GALLAGHER ALENGWA

KIUNGO wa kati wa Chelsea, Conor Gallagher mwenye umri wa miaka 23, anasalia kuwa juu ya orodha ya wachezaji wanaotakiwa na Tottenham huku Spurs hao wakilenga kumnunua kiungo huyo wa kati Januari hii. **(Independent)**

### SALANKE HAUZWI

KLABU ya Newcastle United imeambiwa kwamba mshambuliaji wa England, Dominic Solanke hatauzwa mwezi huu baada ya kufanya uchunguzi kwa ajili ya fowadi huyo wa Bournemouth mwenye umri wa miaka 26. **(Telegraph)**

### DIER ANUKIA BAYERN

KLABU ya Bayern Munich ipo kwenye mazungumzo ya kumsajili mlinzi wa England, Eric Dier mwenye umri wa miaka 29 kutoka Tottenham Hotspur. **(Independent)**

### MARTIAL AMEKATAA

MSHAMBULIAJI wa Manchester United, Anthony Martial amekataa kujiunga na Fenerbahce, Marseille na ligi ya Saudi Pro league, huku Mfaransa huyo mwenye umri wa miaka 28 akitarajiwa kusalia Old Trafford hadi mkataba wake utakapokamilika msimu wa joto. **(Athletic)**

### BERGWIJIN ATAKIWA

KLABU ya West Ham inafikiria kuwasilisha ombi la kutaka kumnunua fowadi wa Ajax, Steven Bergwijn mwenye umri wa miaka 26 na winga wa Sunderland, Jack Clarke mwenye umri wa miaka 23, huku wakitarajia kusajili mchezaji mmoj mwezi huu. **(Telegraph)**

### BRENTFOR PIA WAMUWANIA

BRENTFORD na Crystal Palace pia wanavutiwa na Jack Clarke, ambaye alikuwa Tottenham Hotspur kabla ya kujiunga na Sunderland. **(Evening Standard)**

### SAMARDZIC AWINDWA

KLABU ya Brighton imeingia kwenye kinyang'anyiro cha kumnunua kiungo wa kati wa Serbia, Lazar Samardzic huku Napoli ikiwa imekubali mkataba na Udinese kumnunua mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 21. **(Sky Sports)**

### KILMAN HAUZWI

KLABU ya Wolves haina shinikizo la kumuuza beki wa England, Max Kilman, huku West Ham wakihusishwa na mchezaji huyo wa miaka 26 **(Mail)**

### MEJBRI KWA MKOPO

KLABU ya Sevilla ipo kifua mbele kumsajili kiungo wa kati wa Manchester United na Tunisia, Hannibal Mejbri mwenye umri wa miaka 20 kwa mkopo hadi mwisho wa msimu huu. **(Manchester Evening News)**

### KIWIOR ATAKIWA ARSENAL

KLABU ya Napoli inaweza kumnunua mchezaji wa kimataifa wa Arsenal na Poland, Jakub Kiwior mwenye umri wa miaka 23 na mlinzi wa Chelsea Mfaransa Malang Sarr mwenye miaka 24, huku wakitafuta kumnunua beki wa kati mwezi huu. **(La Repubblica, via Football Italia)**

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# MARTIAL HATAKI KUONDOKA MAN U

### Mfaransa huyo anataka kubaki klabuni hapo mpaka mwisho wa msimu ndipo...

**MANCHESTER, England**

ANTHONY Martial ameripotiwa kukataa wazo la kuondoka Manchester United wakati wa dirisha la usajili la sasa, badala yake ameamua kusalia hadi mwisho wa mkataba wake.

Mshambuliaji huyo ambaye katika miaka ya hivi karibuni uchezaji wake umepungua kutokana na kuwa majeruhi na kukosa kiwango kizuri, ameingia miezi sita ya mwisho ya mkataba wa muda mrefu aliosaini mwaka 2019.

Martial amebadilishwa nafasi yake kwani hivi sasa kocha, Erik ten Hag anapendelea zaidi kumtumia namba tisa Rasmus Hojlund aliyesajiliwa kwa pauni milioni 72, licha ya umri mdogo wa Mdenmark huyo na kukosa mabao kwenye Ligi Kuu.

Lakini badala ya kuangalia kupeleka soka lake kwingine mwezi huu, Sky Sports imeripoti kuwa Mfaransa huyo anataka kubakia.

Inasemekana kwamba Martial amekataa ofa kutoka Marseille na Fenerbahce, pamoja na Ligi Kuu ya Saudia, kwa nia ya kupigania nafasi yake pale United kwa angalau kwa muda mfupi.

90min ilifichua mwezi uliopita kwamba, United hawawezi kuanzisha chaguo katika mkataba wa Martial ambayo una kipengele cha kumuongezea mwaka mwingine hadi msimu wa joto wa 2025.

Hilo halijabadilika, ingawa Ten Hag alikiri hivi majuzi klabu hiyo imekuwa ikizungumza na Martial kuhusu hali ya mkataba wake, angalau akiongeza uwezekano kwamba muda wake Old Trafford hautaisha kama mchezaji huru katika kipindi kifuatacho cha miezi michache.

Martial amestahimili maisha marefu tangu ajiunge na United kwa uhamisho wa pauni milioni 36 kutoka Monaco siku ya mwisho ya uhamisho wa majira ya joto mwaka 2015.

Tangu alipofunga bao lake la kwanza katika ushindi wa Liverpool, aliishia kuchukua kiti cha nyuma kwa Zlatan Ibrahimovic na Romelu Lukaku katika miaka iliyofuata, kabla ya kurudi kwenye ubora wake katika msimu 2019/20.

Lakini, akiwa amefunga mara 23 wakati wa kampeni hiyo pekee, mchezaji huyo hajaweza kuwa kwenye kiwango chake na amezifumania nyavu mara 19 tu kwa United katika mashindano yote ndani ya miaka mitatu na nusu.

HABARI MICHEZO

# MESSI ALIKOSA HESHIMA KWA PSG - AL-KHELAIFI



**PARIS, Ufaransa**

MWENYEKITI wa Paris Saint-Germain, Nasser Al-Khelaifi amemkosoa Lionel Messi kwa kukosa "heshima" kwa klabu hiyo ya Ufaransa baada ya kuondoka kwake Juni 2023.

Nahodha huyo wa Argentina alisema mnamo Septemba kwamba alichukizwa na kwamba PSG haikumheshimu baada ya kubeba Kombe la Dunia.

"Yeye si mtu mbaya, lakini sikupenda," alisema Al-Khelaifi akiiambia RMC Sport.

"Nitasema, sio kwa ajili yake tu bali kwa kila mtu, tunazungumza tukiwa huko, sio tunapokwenda. Hiyo sio mtindo wetu... namheshimu sana Messi, lakini ikiwa mtu anataka kuongea vibaya kuhusu Paris Saint-Germain hiyo si nzuri. Hiyo si heshima."

Messi alifunga mara mbili katika fainali iliyofanyika Qatar na pia akafunga penalti kwenye mikwaju ya penalti huku Argentina ikishinda kwa penalti 4-2 dhidi ya Ufaransa kwenye Kombe la Dunia la 2022.

"Iwapo mtu yeyote atazungumza kuhusu ukweli kwamba hatukumsherehekea vya kutosha baada ya kushinda Kombe la Dunia, tuko Ufaransa na alishinda dhidi ya nyota wa Ufaransa na PSG, Kylian Mbappé," Al-Khelaifi alisema.

"Sisi ni klabu ya Ufaransa. Sitaki uwanja mzima uwe dhidi yake pia."

Al-Khelaifi alikiri kwamba Messi alipata ugumu kuzoea Paris baada ya kuondoka Barcelona msimu wa joto wa 2021.

"Nitasema jambo moja kuhusu Messi, mchezaji bora zaidi duniani na mchezaji bora katika historia," Al-Khelaifi alisema.

"Haikuwa rahisi kwake kuja hapa... Baada ya Barcelona. Huko Barcelona, kila kitu kilikuwa kwa Messi, wachezaji, makocha, na uongozi. Anakuja hapa mambo yalikuwa ni tofauti, tulikuwa na Kylian na pia Neymar."

# Real Madrid yamnyatia Davies

**MADRID, Hispania**

KLABU ya Real Madrid inafuatilia kwa karibu hali ya kimkataba ya Alphonso Davies huko Bayern Munich kwa nia ya kujaribu kumsajili msimu huu wa joto, vyanzo vimeiambia ESPN.

Beki huyo wa kushoto mwenye umri wa miaka 23 anaonekana na klabu hiyo kuwa anafaa kabisa katika kikosi cha Carlo Ancelotti, kutokana na umri wake na ukweli ni kwamba mkataba wake na Bayern unatarajiwa kumalizika Juni 2025.

Vyanzo viliiambia ESPN kwamba tarehe ya kumalizika muda wake ni muhimu kwa nafasi ya dili hilo, kwani Madrid itahamia tu kwa mchezaji huyo wa kimataifa wa Canada ikiwa ataamua kutoongeza, na wababe hao wa Bundesliga watachagua kumfanya apatikane kwa uhamisho badala ya hatari ya kumpoteza bure.

Madrid wana uhusiano mzuri na Bayern na hawataki kuonekana wakiingilia mipango ya klabu hiyo ya Bavaria, lakini wazo lao litakuwa kuiga fomula iliyomfanya kiungo Toni Kroos kuwasili Bernabeu mwaka 2014.

Kroos alikuwa amebakiza mwaka mmoja kwenye mkataba wake na klabu hiyo ya Ujerumani ilimruhusu kusaini Madrid kwa euro milioni 25, badala ya kumuona akiondoka bure mwaka mmoja baadaye.

Kinyume chake, mwaka 2021, Madrid walisubiri hadi mkataba wa beki David Alaba wa Bayern uishe kabla ya kumsajili kama mchezaji huru.

Madrid wanataka kumsajili Davies msimu huu wa joto, kwani kuimarisha beki ya kushoto ni moja ya vipaumbele vya kocha Ancelotti baada ya kuongeza mkataba wake hadi 2026.

Kocha huyo wa Italia Ferland Mendy na Fran García katika nafasi hiyo lakini hakuna anayeshawishi kabisa na ESPN imeripoti kwamba Madrid walikuwa tayari kumwachilia Mendy msimu uliopita wa joto.

Davies amekuwa na kiwango cha juu baada ya miaka mitano ya kuvutia Bayern na anavutia kutua Madrid.

Madrid wana sera iliyoanzishwa ya kulenga vipaji bora chini ya umri wa miaka 25, na vilevile umri wake na uwezo wa Davies - wa kucheza pande zote mbili na mbele zaidi - inaweza kuonekana kama faida nyingine. Kikwazo kikubwa zaidi kitakuwa Bayern kumshawishi mchezaji huyo kuongeza mkataba wake.

Vyanzo viliiambia ESPN kwamba Davies anaweza kuwa na nia ya kuhama na anavutiwa na mradi wa michezo wa Madrid, lakini pia yuko tayari kusikia toleo la mwisho la Bayern.

# Palmer hakutaka kuondoka Man City

**LONDON, England**

COLE Palmer amekiri kuwa hakuwa na nia ya kuondoka Manchester City kwa misingi ya kudumu, lakini alinyimwa nafasi ya kutoka kwa mkopo kabla ya uhamisho wake wa pauni milioni 40 kwenda Chelsea.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 21 alifurahia kampeni ya mafanikio akiwa na Man City wakati wa msimu wao wa kushinda mataji matatu wa 2022/23, ingawa kwa kiasi kikubwa hakucheza akitokea benchi.

Palmer hakuhusishwa na kuondoka Man City hadi mwishoni mwa dirisha la majira ya joto baada ya kufunga katika mechi yao ya waliyopoteza kwenye Ngao ya Jamii dhidi ya Arsenal na ushindi wa UEFA Super Cup dhidi ya Sevilla, ambapo mustakabali wake wa muda mrefu ulitiliwa shaka.

Akizungumza na Sky Sports kabla ya Jumanne kufungwa 1-0 na Middlesbrough katika mechi ya kwanza ya nusu fainali ya Kombe la Carabao, Palmer alifichua kuwa alikuwa na nia ya kubakia Man City, lakini sasa ana furaha Chelsea.

"Jambo langu lilikuwa ni kutowahi kuondoka City, hiyo haikuwa nia yangu, nilitaka kwenda kwa mkopo kwa mwaka mmoja, nirudi na kuwa tayari kwa kikosi cha kwanza. Lakini walisema siwezi kwenda kwa mkopo, nibaki kuuzwa," alisema Palmer.

"Hivyo basi, Chelsea walinipigia simu na nina furaha sana kuwa hapa. Nina furaha sana nilifanya uamuzi bora wa kuja hapa."

Ingawa Chelsea imekuwa na matatizo makubwa msimu huu, Palmer amejitangaza kuwa mmoja wa wachezaji chipukizi bora zaidi nchini humo, akiwa amefunga mabao nane na kutoa pasi nne za mabao katika mechi 16 za Ligi Kuu England hadi sasa. Pia amecheza mechi yake ya kwanza ya England tangu ajiunge na The Blues hao.

Kocha mkuu wa Chelsea Mauricio Pochettino amemfananisha Palmer na gwiji wa Argentina, Angel Di Maria - ulinganisho ambao Mwingereza huyo mchanga anafurahishwa nao.

HABARI MICHEZO

# CHE MALONE: TUNAKOSA UMAKINI UWANJANI

**Na Saada Akida**

BEKI wa Simba, Che Fondoh Malone amefunguka kuwa safu yao ya ulinzi imekuwa na umakini mdogo uwanjani lakini anaamini kocha wao Abdelhak Benchikha atalifanyia kazi suala hilo kabla ya kurejea katika Ligi Kuu Tanzania Bara na Ligi ya Mabingwa Afrika katika hatua ya makundi.

Amesema umakini mdogo ndio uliowafanya waruhusu bao katika dakika za mapema katika mchezo wa juzi wa nusu fainali ya kombe la Mapinduzi Zanzibar dhidi ya Singida Fountain Gate FC.

Simba juzi walifanikiwa kutinga fainali ya michuano hiyo kwa mikwaju ya penalti 3-2 baada ya kufungana bao 1-1 katika dakika 90 za mchezo.

Akizungumza na Nipashe jana, Che Malone alisema Singida ni timu kubwa na wana wachezaji wazuri ambao waliwapa ushindani mkubwa zaidi ya ilivyo katika mechi yao iliyopita ya Ligi Kuu Tanzania Bara.

Alisema kila wanapokutana na Singida Fountain Gate FC unakua mchezo wenye ushindani na mgumu kutokana na ubora wa wachezaji.

„Mpira dakika 90, hatukutakiwa kukata tamaa, tulipoteza umakini na wapinzani wakafanikiwa kupata bao dakika ya mwanzo, wana timu nzuri kwa kuwa tulihitaji matokeo tumepambana na kufanikiwa kufikia malengo yetu ya kucheza fainali," alisema beki huyo.

Aliongeza kuwa baada ya mchezo huo kocha Abdelhak Benchikha ameona mapungufu ya kikosi chake na atayafanyia kazi kabla ya kwenda kucheza mchezo wao wa fainali na michezo mingine iliyopo mbele yao ikiwemo Ligi Kuu na michuano ya kimataifa.




Meneja Mawasiliano wa Kampuni ya Simu za Mkononi ya Airtel, Jackson Mmbando (katikati), Meneja Masoko wa Tecno, Salma Shafii na Meneja Data wa Airtel, James Gua, wakipuliza mavuvuzela, kuashiria uzinduzi wa kampeni ya Upige Mwingi Mpaka Afcon, ambayo wateja wa Airtel watajishindia tiketi za kushuhudia nusu fainali za mashindano hayo nchini Ivory Coast. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wateja Airtel kushuhudia AFCON

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI ya Airtel kwa kushirikiana na Tecno jana wamezindua rasmi kampeni kabambe ya kuwapeleka wateja wake kushuhudia michezo ya nusu fainali ya fainali ya Mataifa ya Afrika (AFCON).

Fainali hizo za AFCON zinatarajiwa kuanza kesho nchini Ivory Coast huku timu ya taifa ya Tanzania 'Taifa Stars' ikiwa miongoni mwa timu zitakazoshiriki fainali hizo.

Akizungumza kwenye uzinduzi huo, Meneja wa Mawasiliano wa Airtel, Jackson Mbando alisema wateja watapata fursa pia ya kushinda zawadi mbalimbali kutoka katika makampuni hayo.

"Airtel tunaanza Mwaka Mpya wa 2024 kwa kishindo! Ushirikiano wetu na TECNO katika 'Promosheni ya 'Upige Mwingi Mpaka AFCON' ni kuhakikisha wateja wetu wanapata burudani ya soka sambamba na amsha amsha za msisimko wa burudani za AFCON 2024. Tunawaalika wateja wetu kushiriki mara nyingi wanavyoweza na kupata nafasi ya kushinda zawadi kabambe," alisema Jackson.

Alisema wateja wa Airtel wanaweza kujiunga na kampeni hiyo kupitia huduma ya Airtel Money.

Kwa upande wake, Meneja wa Tecno, Salam Shafii, alisema kampuni yake ndio mdhamini mkuu wa fainali hizo na wameamua kuungana na Airtel hapa Tanzania kuwapa fursa mashabiki za kushuhudia faianli hizo Ivory Coast.

"Tecno kama mdhamini rasmi wa Afcon 2024 inafurahi kushirikiana na Airtel kuwapa wateja wa Airtel nafasi ya kuwa sehemu ya mashindano ya Afcon 2024. Tunafurahi kuwa sehemu ya familia ya zaidi ya wateja milioni 17 wa Airtel na kuwapa nafasi ya kwenda kushuhudia fainali za AFCON," alisema Salma.

Zawadi nyingine zitakazotolewa kwenye kampeni hiyo ni bodaboda , televisheni, simu za mkononi pamoja na friji.

## Rais Samia achangia Shilingi milioni 500

INATOKA UK. 24

Serikali bali ni ushirikiano wa taasisi na mashirikisho mbalimbali . Wito wangu kila shirikisho kuweka mpango kazi kwa ajili ya kutengeneza fursa kwa vijana wetu . Harambee hii tumepata mafanikio nawasihi wale wote walioahidi kutimiza ahadi zao kwa wakati," alisema Waziri Mkuu.

Katika hatua nyingine jezi ya golikipa wa zamani wa Taifa Stars , Juma Pondamali imeweka rekodi ya mauzo makubwa ikiuzwa shilingi milioni 25, kwenye mnada maalum uliofanyika katika hafla hiyo.

Mnada huo ambao uliendeshwa na Waziri Mkuu Majaliwa katika hafla hiyo kwa kuuza jezi za wachezaji wa zamani wa Taifa Stars wakiwemo wale ambao walishiriki michuano ya Afcon mwaka 1980 nchini Nigeria, Tanzania ikishiriki kwa mara ya kwanza.

Jezi ya kwanza kuuzwa kwenye mnada huo maalum kwa wadau wa michezo nchini wakiwemo wakuu wa tasisi na makampuni ilikuwa ni jezi ya kipa Juma Mkambi iliyouzwa kwa dau la shilingi milioni moja na nusu.

Lakini jezi ya Athuman Chama iliuzwa kwa shilingi milioni sita sawa na jezi ya aliyekuwa nahodha wa timu ya taifa iliyofuzu kwa mara ya kwanza AFCON mwaka 1980, Leodgar Chila Tenga huku Mamlaka ya Bandari Tanzania TPA ikinunua jezi ya Pondamali kwa dau la shilingi milioni 25.

## Yanga yarejea mazoezini kujiwinda Ligi ya mabingwa

INATOKA UK. 24

itakuwa na kibarua kizito Februari 23 dhidi ya CR Belouizdad ya Algeria kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam, kabla ya Machi Mosi kusafiri mpaka Misri kucheza dhidi ya Mabingwa Watetezi, Al Ahly ya Misri.

Yanga ipo Kundi D ikiwa na pointi tano kama Al Ahly inayoongoza kundi hilo, lakini iko nafasi ya pili kwa tofauti ya mabao ya kufunga na kufungwa.

Kwa upande wa Ligi Kuu Tanzania Bara, ratiba inaonyesha kuwa itarejea tena dimbani kwa mara ya kwanza baada ya kumalizika kwa fainali za AFCON, Februari 18 itakapokipiga dhidi ya JKT Tanzania.

Kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara, Yanga pia ipo nafasi ya pili kwenye msimamo ikiwa na pointi 30, juu yake ikiwa Azam FC ambao ndiyo vinara wa ligi kwa sasa, wenye pointi 31.

==

Michezo


Ijumaa Januari 12, 2024

Nipashe

## Martial hataki kuondoka Man United

UKURASA 21






Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa (kushoto),akikabidhi jezi ya timu ya taifa yenye jina la aliyekuwa kocha wa timu hiyo marehemu Joel Bendera kwa Katibu Mkuu Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi,Vijana,Ajira na Watu Wenye Ulemavu), Mhandisi Cyprian Luhemeja (wapili kushoto), wengine ni Mkurugenzi Mkuu wa PSSSF, Hosea Kashimba (watatu kushoto) na Meneja Uhusiano na Elimu kwa Wanachama PSSSF, James Mlowe. **PICHA: MPIGA PICHA WETU**

# RAIS SAMIA ACHANGIA SHILINGI MILIONI 500 KWA TIMU ZA TAIFA

## ●●●Ni katika harambee iliyosimamiwa na Waziri Mkuu, wakusanya shilingi milioni.....

**Na Saada Akida**

RAIS Samia Suluhu Hassan juzi amechangia jumla ya shilingi milioni 500 katika Harambe ya kuzichangia timu za taifa iliyosimamiwa na Waziri Mkuu, Kasim Majaliwa huku makusanyo na ahadi zote zikifikia Sh Bilioni 3.7.

Hafla ya Harambee hiyo iliandaliwa na Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo chini ya Waziri wake, Dk. Damas Ndumbaro ikiwa inalenga kuzisaidia timu zote za taifa ikiwemo, Taifa Stars inayoshiriki michuano ya mataifa Afrika (Afcon) nchini Ivory Coast, Twiga Stars inayotarajia kushiriki michuano ya Mataifa Afrika kwa Wanawake (WAFCON) ambayo imepangwa kufanyika mwaka huu nchini Morocco.

Timu nyingine ni pamoja na timu ya taifa ya ngumi, timu ya taifa ya soka kwa watu wenye ulemavu (Tembo Warriors) pamoja na nyingine zote za taifa.

Hafla hiyo ilifanyika juzi kwenye Hoteli ya Johari Rotana jijini Dar es Salaam ambapo harambe ya uchangiaji iliongozwa na Waziri Mkuu kabla ya Rais Samia kufungua uchangiaji kwa njia ya simu kwa kutoa shilingi milioni 500.

Rais Samia alisema kuwa michezo ni jukumu la kila mmoja nchini na Serikali itaendelea kusimamia michezo mbalimbali hasa kutokana na gharama kubwa ya uendeshaji michezo.

„Tuna ufinyu wa bajeti, naomba wadau mbalimbali katika sekta hii kuchangia timu zetu ili kuzifanya ziende kwenye kushindana kwenye mashindano mbalimbali na si kushiriki tu, tuchangie timu zetu, kwa kuanzia...., mimi na marafiki zangu tutachangia shilingi milioni 500 ambayo ni utangulizi.

„Naomba tuchangia timu zetu kusaidia Serikali kwa sababu michezo ni yetu wote, tegemeo langu Watanzania kutuunga mkono Serikali katika kuendeleza michezo hapa nchini,“ alisema Rais Samia katika hotuba yake fupi aliyoitoa kwa njia ya simu.

Kwa upande wa Waziri Mkuu Majaliwa alisema “Nawashukuru wadau wa michezo kwa zoezi letu la harambee kuanzia mwanzo hadi sasa na jumla ya fedha za harambee zilizotolewa na ahadi ni shilingi bilioni 3.7 .

„Kwa ukanda wa CECAFA, Tanzania inaanza kujulikana jitihada zimeonekana katika soka, ngumi na riadha siyo kwa

INAENDELEA UK. 23

# Yanga yarejea mazoezini kujiwinda Ligi ya mabingwa

**Na Adam Fungamwango**

SIKU chache baada ya kuondolewa kwenye michuano ya Kombe la Mapinduzi, kikosi cha Yanga kimepanga kurejea mazoezini huku Kocha Miguel Gamondi akisema kwa sasa wanageukia mashindano ya kimataifa.

Miguel alisema baada ya michuano hiyo ya Mapinduzi, amewapumzisha wachezaji wake na watarejea tena Jumatatu na kuanza maandalizi ya michuano inayofuata, hasa mechi dhidi ya CR Belouizdad na Al Ahly ya Ligi ya mabingwa Afrika hatua ya makundi.

„Vijana nimewapa mapumziko, tutarejea tena Jumatatu kwa ajili ya mazoezi kwani tuna vita ngumu mbele yetu, hasa michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika kwa hiyo ni lazima tujiandae kisawa sawa, najua pia kutakuwa na mechi za Ligi Kuu Tanzania Bara, lakini akili yetu ipo kwenye Ligi ya Mabingwa Afrika zaidi,“ alisema Gamondi

Alisema mashindano ya mapinduzi yamemsaidia kwa kiasi kikubwa kuwapa nafasi wachezaji wake ambao walikuwa hawapati nafasi kwenye kikosi cha kwanza na ameona uwezo wao.

Alisema wapo wachezaji ambao wameonyesha uwezo mkubwa na wanaweza kuaminika kwenye kikosi hicho katika michezo ijayo ya timu hiyo.

„Tumeondolewa Mapinduzi lakini kipo nilichokiona kwa wachezaji wangu, mashindano haya yamenipa mwanga mkubwa juu ya wachezaji wangu,“ alisema Gamondi

Yanga ambayo Jumamosi iliyopita ilitolewa kwenye hatua ya robo fainali ya Kombe la Mapinduzi dhidi ya APR ya Rwanda,

INAENDELEA UK. 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >